SportPesa
JACKPOT BABA LAO!
TZS. 253,545,950
CHEZA SASA KWA 1000/= TU!
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



UKURASA 4

**RAIS SAMIA**: Serikali iongoze, sekta binafsi itafanya biashara




UKURASA 11

# Nipashe

Jumatano Juni 15, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580977
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Kicheko walalahoi, kilio kwa vigogo

UKURASA 2, 3 & 4







Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba

Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar, Saada Mkuya

**MICHEZO** **YANGA YAPANIA UBINGWA LEO** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Ni bajeti ya kubana matumizi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetaja maeneo kadhaa katika mwaka 2022/23 itakayobana na kuondoa matumizi yasiyo ya lazima, ikiwamo kupimiana mafuta, kubana matumizi ya magari ya serikali kwa baadhi ya watumishi wa umma na kuminya safari za nje na ndani.

Akiwasilisha mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya serikali kwa mwaka huo, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema serikali inatarajia kudhibiti ununuzi na matumizi ya magari kwa kuzingatia Waraka wa Rais namba moja wa mwaka 1998 kuhusu hatua za kubana matumizi ya Serikali na Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma namba mbili wa mwaka 2021 kuhusu utaratibu wa kutumia magari, aina na stahili za magari kwa viongozi katika utumishi wa umma ili kubana matumizi.

"Baadhi ya maeneo yenye gharama kubwa sana kwa serikali ni ununuzi wa magari, ununuzi wa mafuta ya uendeshaji, ununuzi wa vipuri na matengenezo," alisema. Alibainisha kuwa serikali inatarajia kukusanya na kutumia Sh. trilioni 41.48 kwa mwaka 2022/23. Kati yake, mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa Sh. trilioni 28.02, sawa na asilimia 67.5 ya bajeti yote, mapato yatakayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yanakadiriwa kuwa Sh. trilioni 23.65 na mapato yasiyo ya kodi (Wizara, Idara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa) yanakadiriwa kuwa Sh. trilioni 4.37.

Kwa mujibu wa waziri huyo, misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo inatarajiwa kuwa Sh. trilioni 4.65, sawa na asilimia 11.2 ya bajeti yote, huku serikali ikitarajia kukopa Sh. trilioni 5.78 kutoka soko la ndani ambapo Sh. trilioni 3.30 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za serikali zinazoiva na Sh. trilioni 2.48 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Vilevile, alisema serikali inatarajia kukopa Sh. trilioni 3.03 kutoka soko la nje kwa masharti ya kibiashara kwa lengo la kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**KUBANA MAFUTA**

Hatua za muda mfupi zitakazochukuliwa ni kupunguza safari za ndani na nje, kukata fedha za ununuzi usio wa lazima, kupunguza ukubwa wa uwakilishi kwenye mikutano ya ndani na nje, na kupima mafuta ya magari ya serikali kila mwezi kufuatana na shughuli za lazima.

**MIKOPO YA MAGARI**

Hatua za muda wa kati na mrefu, alisema serikali inapendekeza kubadili utaratibu uliopo kwa kuwakopesha magari watumishi wenye hadhi ya kuwa na gari la serikali wawe na magari yao, wafanye matengenezo, wanunue vipuri na masuala ya mafuta yaangaliwe kwa utaratibu utakaoonekana unafaa.

"Kwa sasa serikali inatumia zaidi ya Sh. bilioni 558.45 kwa mwaka kwa ajili ya ununuzi wa magari, mafuta ya uendeshaji, ununuzi wa vipuri na matengenezo."

Alisema hatua hiyo itaondoa utaratibu uliozoeleka, dereva na gari anapitishwa chini, bosi anapanda ndege mpaka Mwanza au Mbeya kutoka Dar es Salaam na kurudi hivyo hivyo.

**UTAFITI**

"Kuna utafiti wa siri ulifanywa, kwa siku moja yalibainika magari ya serikali yaliyotoka Dodoma kwenda Dar es Salaam yalikuwa 132, na yaliyokuwa yanatoka Dar es Salaam yakipishana kuja Dodoma yalikuwa 76, na mengine nane yalikuwa yamepinduka. Je kwa mwezi ni gharama kiasi gani?"

**MABILIONI KUOKOLEWA**

Alisema kwa utaratibu huo gharama za matumizi ya magari serikalini ni Sh. bilioni 50.5 na zaidi ya Sh. Bilioni 500 zitaokolewa na kuelekezwa kwenye ununuzi wa dawa muhimu hospitalini, kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaosoma vyuo vya kati, na kutekeleza miradi ya maendeleo.

**MFUMO WA UNUNUZI**

Serikali itaachana na mfumo wa sasa wa ununuzi wa umma ambao umeshindwa kuleta tija kwa kuwa msingi wake mkubwa ni ulinganishaji wa zabuni zilizofunguliwa badala ya bei za bidhaa na huduma.

"Sasa serikali ni moja, bidhaa zinafanana, hata ofisi zilizoko mkoa mmoja, ila inatokea kila mmoja anakuwa na bei zake licha ya bidhaa kufanana," alisema.

Alisema serikali itaendelea kuboresha Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (TANePS), ikiwamo kuweka ukomo wa bei za bidhaa na huduma zinazotumika serikalini ili kudhibiti matumizi ya fedha za serikali.

Alisema Wizara hiyo itatoa Waraka wa Hazina kuelekeza idara na taasisi kununuzi kununua bidhaa zinazofanana kwa bei ya kikomo na endapo kutakuwa na ulazima wa kununua magari kwa wingi, serikali itafanya mazungumzo na Toyota Tanzania na Japan (kwa njia za kidijitali) ili kufanya makubaliano ya jumla ili Serikali kupata bei nafuu kama ilivyo kwa mashirika makubwa ya kimataifa kama vile UNDP.

Pia alipendekeza matumizi ya mifumo ya TEHAMA iwe chaguo namba moja katika utekelezaji wa shughuli za serikali ili kubana matumizi na kuanzia mwaka ujao wa fedha ofisi za serikali zianze 'paperless operations' kwenye shughuli zake.



Msafara wa gari alilopanda Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, ukiwasili katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAJIM JOSEPH**

## CAG aongezwa nguvu kiutendaji

**Na Jenifer Gilla**

SERIKALI imesema itaendelea kumpa nguvu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ili kumwezesha kukagua thamani ya fedha kwenye miradi yote mikubwa na kufanya ukaguzi kwa wakati.

Akiwasilisha bungeni jana hotuba yake kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya serikali kwa mwaka 2022/ 23, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema hatua hiyo inakwenda sambamba na kumwongezea fedha ili aajiri watumishi wa kutosha.

"Ninapendekeza kumwongezea fedha CAG ili apate watumishi wa kutosha kwa kuajiri na kuwahamisha watumishi kutoka idara yoyote ya serikali na kuwajengea uwezo kwa mafunzo na weledi wa ukaguzi wa thamani ya fedha," alisema.

Alitaja hatua nyingine ni kufanya marekebisho Sheria ya Ununuzi wa Umma ili kuziba mianya inayotoa fursa ya miradi kutekelezwa bila kujali thamani ya fedha kama alivyoelekeza Rais Samia Suluhu Hassan. Pia alisema serikali itaendelea kuimarisha vitengo vya ukaguzi wa ndani kwa kuvijengea uwezo wa kitaaluma na kuongeza idadi ya watumishi katika fani mbalimbali kama vile TEHAMA, uhandisi, ukadiriaji majenzi, wakemia wanasheria na fani nyingine ili kuondokana na dhana ya wakaguzi wa ndani kuwa na taaluma ya fedha pekee.

Waziri huyo alisema serikali itafanya marekebisho ya Kanuni za Fedha za Umma kwa kuziwezesha kamati za ukaguzi kuwa na wajumbe wa nje watatu ikiwamo Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi ili kuongeza uhuru na ufanisi wa kamati za ukaguzi.

"Pamoja na mambo mengine, marekebisho ya kanuni hizo yatazitaka Kamati za Ukaguzi kuwasilisha taarifa za ukaguzi wa ndani kwa Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali kila robo mwaka," alisema.

Vilevile, alipendekeza Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali kuwa na fungu lake pamoja na kuongeza idadi ya wakaguzi wa ndani ili kuimarisha na kuboresha ufanisi katika utendaji.

"Kuna wakati inatokea tunaona miradi ikikamilika, fedha zote zikiwa zimetumika lakini miradi ikiwa chini ya viwango, jengo au mradi unakamilika ungali bado ananukia rangi, lakini ukiwa umetapakaa nyufa kila kona, simenti na matofali yakiwa ni mchanga," alisema.

# Utaratibu mpya wa kupata mabosi SU

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imetangaza utaratibu mpya wa kuwapata wakuu wa mashirika ya umma, maarufu SU, ikibainishwa kuwa kuanzia sasa wataanza kufanyiwa usaili kwa ushindani badala ya kuteuliwa.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba alitangaza utaratibu huo jana bungeni jijini Dodoma wakati akisoma hotuba ya mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya serikali kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Dk. Mwigulu alisema: "Ninapendekeza wakuu wote wa mashirika ya umma wafanyiwe usaili kwa ushindani. Ninapendekeza nafasi zianze kutangazwa punde nafasi ikiwa wazi ili wenye sifa wajitokeze na wafanyiwe usaili na iwe hivyo hivyo kwa bodi."

Alisema wenye sifa ndiyo wafanyiwe upekuzi kufanyiwa uteuzi na kupewa mkataba wenye malengo yanayopimika.

**UKITUMBULIWA, MSHAHARA...**

Dk. Mwigulu alisema kuanzia mwaka ujao wa fedha, kiongozi wa serikali wakiwamo makatibu wakuu, manaibu, wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya, wakurugenzi watendaji wa halmashauri, makatibu tawala wa wilaya, wakurugenzi, wakuu wa taasisi mbalimbali, wakuu wa idara mbalimbali pindi wanapotumbuliwa na kupangiwa majumu mengine, watalipwa mishara yao kwa viwango vya zamani.

"Viongozi hao napendekeza yeyote aliyetokea kwenye nafasi yake ya kuteuliwa akitolewa na akabaki kwenye utumishi wa umma arejee pia kwenye mshahara wake wa zamani ili kuwapunguzia Watanzania mzigo wa kuwalipa watu waliokaa benchi huku wakiziba nafasi za vijana wapya kuajiriwa," alisema.

Dk. Mwigulu alisema tangu uhuru viongozi wakitenguliwa huendelea kulipwa mshahara ule ule sawa na aliyeko kazini mpaka anastaafu.

**BAJETI YA SERIKALI 2022/23**

# Elimu bure sasa hadi kidato cha 6

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imependekeza kufuta ada kwa kidato cha tano na cha sita ili kuwapunguzia gharama wanafunzi.

Hatua hiyo ina maana kwamba ada sasa haitokuwapo kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha sita baada ya serikali kuanza kutekeleza Mpango wa Utoaji Elimumsingi Bila Malipo, maarufu elimu bure, mwaka 2016.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alipendekeza kufuta ada hiyo alipowasilisha bungeni jijini Dodoma jana mapendekezo ya serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya serikali kwa mwaka 2022/23.

Alisema kwa sasa wanafunzi wa kidato cha tano ni takribani 90,825 na kidato cha sita ni 56,880 na mahitaji ya fedha ni Sh. bilioni 10.339.

"Ili kuwapunguzia gharama watoto hawa, kama Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan alivyoielekeza wizara, ninapendekeza kufuta ada kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita.

"Kwa hatua hii, elimu bila ada ni kuanzia shule za msingi mpaka kidato cha sita. Serikali itajipanga kuangalia namna ya kusaidia vyuo vya kati kadiri hali ya uchumi itakavyotengemaa," Dk. Mwigulu alisema huku akijikuta amekiuka Kanuni za Bunge alipowahoji wabunge wenzake 'nani kama Samia?'

Waziri Dk. Nchemba alisema serikali imeendelea kugharamia Programu ya Elimumsingi Bila Ada ambapo hadi Aprili mwaka huu, Sh. bilioni 244.5 zilitolewa.

Alisema Rais Samia ameguswa na watoto kukatisha masomo kutokana na sababu mbalimbali, miongoni mwake zikiwa umaskini wa kipato kwenye familia, mimba za utotoni, mwamko duni wa elimu kwa baadhi ya jamii, utoro na wasioendelea kwa mujibu wa sheria (ufaulu duni).

Alisema ili kukabiliana na mimba za utotoni, serikali itaendelea kujenga



mabweni kwenye maeneo hatari kwa watoto wa kike.

Waziri huyo alisema ili kutoa fursa kwa watoto wasioendelea na vidato na vyuo, serikali itaendelea kuimarisha elimu ya ufundi hususan katika vyuo vya kati kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kujiajiri ama kuajiriwa.

"Mpaka sasa, wilaya 77 zina Vyuo vya Ufundi VETA kati ya wilaya 138 nchini kote. Tuna mikoa 25 ina VETA kati ya mikoa 26. Bado Mkoa wa Songwe hauna kabisa VETA na wabunge wa mkoa wa Songwe wamekuwa wakishinda ofisini wakifuatilia ahadi waliopewa na Mheshimiwa Rais.

"Bado kuna wilaya 36 ambazo hazina vyuo wala vyuo vya mkoa. Ninapendekeza kutoa Sh. bilioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa vyuo vya ufundi kwa Mkoa wa Songwe na wilaya 36 ambazo hazina vyuo ili kufanya wilaya zote 138 kuwa na VETA," aliwasilisha.

## Rais Samia: Serikali iongoze, sekta binafsi ifanye biashara

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema tangu aingie ofisini, sera yake imekuwa kuifanya serikali iongoze na sekta binafsi ifanye biashara.

Mkuu wa Nchi alitoa kauli hiyo juzi Muscat, Oman aliposhiriki kongamano la wafanyabiashara wa Oman na Tanzania na kushuhudia utiaji saini makubaliano ya ushirikiano wa pamoja katika sekta mbalimbali. Akiwa huko kwa ziara ya kikazi, Rais Samia alisema Tanzania ina nia ya dhati ya kuhakikisha sekta binafsi inaendesha uchumi.

Rais alisema serikali inaendelea kuhakikisha inaboresha mazingira ya biashara kwa kushirikiana na sekta binafsi na wanaendelea kuweka sera rafiki kwa wafanyabiashara ili kufikia malengo waliyojiwekea.

"Tangu niingie ofisini, sera yangu imekuwa kuifanya serikali iongoze na wafanyabiashara wafanye biashara na ninamaanisha kwa kusema hivi.

"Serikali haitafanya biashara tena, suala la biashara tunaiachia sekta binafsi. Sisi serikalini kazi yetu ni kutengeneza mazingira rafiki ya kuwezesha wafanyabiashara wa ndani na nje kufanya biashara zao," alisema.

**BAJETI ZANZIBAR**

# Wamiliki kampuni za mtandao kuanza kulipa VAT

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAMILIKI wa kampuni za mtandaoni wataanza kulipa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), kuanzia mwaka ujao wa fedha ili kuongeza mapato ya serikali.

Akiwasilisha Bajeti Kuu ya Serikali ya Zanzibar katika Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum, alisema serikali inakusudia kukusanya Shilingi bilioni sita katika eneo hilo.

Alisema hatua hiyo inalenga kurahisisha utaratibu wa usajili wa walipakodi wanaotoa huduma za kidijitali bila ya kuwa na makazi nchini.

Mkuya alisema, serikali pia itaongeza unafuu wa kodi ya ongezeko la thamani kutoka asilimia 80 hadi 100 kwa mwekezaji asiyekuwa wa kimkakati wakati wa ununuzi wa bidhaa nchini kwa ajili ya ujenzi. Alisema hatua hiyo itakwenda sambamba na marekebisho ya kupunguza unafuu wa VAT kutoka asilimia 80 hadi 75 wakati wa uingizaji wa bidhaa nchini.

Aidha, alisema kutokana na uwajibikaji mdogo kwa walipakodi wanaofanya biashara za gari, serikali itapunguza viwango vya kutozea ushuru wa stempu kwa gari za biashara kwa asilimia 25 ili kuongeza uwajibikaji, ulipaji kodi wa hiari na kuleta ufanisi katika usimamizi wa mapato.

Alisema ili kudhibiti mapato yatokanayo na bidhaa ya gesi asilia, serikali imeondoa utozaji ushuru wa stempu kwa bidhaa ya gesi asilia na kuweka utaratibu wa kutoza tozo ya petroli katika bidhaa hiyo wakati wa uingizaji kama ilivyo kwa mafuta.

**VIPAUMBELE**

Katika bajeti hiyo, Mkuya alitaja vipaumbele sita vitavyotekelezwa kwa mwaka ujao wa fedha ikiwamo kuimarisha huduma za jamii, matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika utoaji wa huduma, maslahi ya watumishi wa umma na kutekeleza miradi ya kimkakati.

Aidha, kuimarisha misingi ya utawala bora na maadili, kupambana na udhalilishaji na kuitangaza Zanzibar kiutalii.

Alisema kwa mwaka ujao wa fedha, serikali imetenga Sh. bilioni 628.68 sawa na asilimia 24 ya bajeti kwa ajili ya mishahara ya wafanyakazi yakiwamo marekebisho mapya ya mishahara.

Alisema serikali pia itaanza kulipa mishahara kwa madiwani ili watekeleze majukumu yao ya kusimamia wananchi na kuanzisha fao la kupoteza ajira.

Pia, serikali itatekeleza miradi 13 ya kimkakati ambayo itabadilisha taswira ya Zanzibar, kukuza uchumi, kuimarisha huduma za jamii na kuongeza fursa za ajira, Sh. bilioni 798 zimetengwa kutekeleza miradi hiyo.

Alisema serikali itaanza kutoza kodi ya miundombinu kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye vileo wakati wa uingizaji nchini. Aidha, alisema kianzio hicho kitajumuishwa katika vianzio vya kodi ya miundombinu, ambapo asilimia 50 ya mapato yatatumika kwa ajili ya kuongeza ufanisi.

Kwa mwaka ujao wa fedha, serikali itatumia Sh. trilioni 2.59 na asilimia 53 ni kwa miradi ya maendeleo, asilimia 24 mishahara ya watumishi wa umma, asilimia 15 kwa ajili ya kuendesha ofisi na asilimia nane kwa ajili ya huduma za mfuko mkuu wa serikali.

Yetu Microfinance Bank PLC

**TANGAZO**

**KWA WALIOWAHI KUWA WAFANYAKAZI WA YETU MICROFINANCE BANK PLC**

**YETU MICROFINANCE BANK PLC** Inawatangazia waliowahi kuwa wafanyakazi wake na kuacha kazi huku wakiwa na madeni ya mikopo waliyochukua wakiwa wafanyakazi, wafike kwenye matawi ya Benki hiyo popote yalipo au makao makuu ya benki hiyo hili kufanya makubaliano ya namna gani wataweza kulipa madeni ya mikopo yao. Benki inawataka kufanya hivyo ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya Tangazo hili. Kinyume na hapo Benki itatoa majina pamoja na picha zao gazetini ikifuatiwa na hatua kali za kisheria kuchukuliwa dhidi yao.

216903401

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA U J E N Z I , UCHUKUZI NA**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
21.03.2022

**TANGAZO**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **14.06.2022** hadi **27.06.2022** kampuni ya **Spedag Interfreight** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Holili kuelekea Moshi**, gari hilo lenye namba za usajili:

**KCJ943F/ZE1097, KCM104W/ZF0174**
**KBQ622Z/ZE0978, KCK293W/ZE2585**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo
**Urefu - Mita 21** **Upana - Mita 4.15** **Kimo - Mita 5.15**

3. Njia itakayotumika: **Holili** hadi **Moshi** kupitia **Soweto**, gari litasafiri muda wa mchana tu (**Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni**)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

216998001

# Unafuu petroli na mafuta ya kula waja

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

NI bajeti ya kubana matumizi! Ndivyo unavyoweza kusema baada ya Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, kupendekeza na kuonyesha maeneo ambayo serikali itabana matumizi ili kuwapunguzia mzigo Watanzania.

Katika kuleta nafuu ya maisha serikali imepanga kupunguza tozo mbalimbali kwenye mafuta ya petroli na dizeli pamoja na mafuta ya kula ili kuwawezesha Watanzania kumudu bidhaa hizo.

Serikali imependekeza kuondoa kodi kwenye mashine za kielektroniki katika ukusanyaji mapato (EFD) ili kuwezesha wafanyabiashara kuwa nazo kwa wingi na serikali iendelee kupata mapato.

Waziri Nchemba alitumia saa mbili na dakika 27 kuwasilisha mapendekezo hayo bungeni jijini hapa jana, akibainisha hatua za makusudi ili kupunguza tozo mbalimbali zilizokuwa kwenye ukokotoaji wa bei ya nishati ya mafuta.

"Serikali inachukua hatua nyingine katika suala hili ikiwamo: Kuendelea kutoa ruzuku kwa ajili ya kupunguza bei ya nishati ya mafuta; kuruhusu watu wenye uwezo wa kuleta mafuta wa bei nafuu.

"Pia kuanzisha mfuko wa kuhimili ukali wa bei za mafuta baada ya bei za mafuta kutulia katika soko la dunia; kuanzisha hifadhi ya mafuta ya kimkakati na kuanzisha upokeaji wa mafuta katika ghala," alisema.

Kuhusu mafuta ya kula, Dk. Nchemba alisema serikali inapendekeza kuweka mikakati ya kikodi ili kutoa unafuu wa uagizaji wa mafuta ghafi ya kula kwa wachakataji wa ndani kwa lengo la kuongeza uzalishaji, kupunguza bei ya bidhaa hiyo na kuongeza ajira.

"Wakala wa Taifa wa Uzalishaji na Uendelezaji wa Mbegu za Kilimo imesafisha na kusambaza kwa wakulima tani 2,000 za mbegu za alizeti zenye thamani ya Sh. bilioni 5.84 kwa utaratibu wa ruzuku kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula na kwamba wastani wa tani 400,000 za alizeti na tani 100,000 za mafuta zinatarajiwa kuzalishwa," alisema.

**NYWELE BANDIA**

Alisema nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) zimekubaliana kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 35 kwenye nywele bandia zinazotambulika kwa Heading 6704.

Alisema hatua hiyo inalenga kulinda wazalishaji wa ndani wa bidhaa hizo, kuongeza ajira pamoja na kuongeza mapato ya serikali.

**KODI SIMU JANJA**

Waziri Mwigulu alisema serikali inapendekeza kufuta msamaha wa Kodi ya VAT kwenye simu janja (Smartphones) HS code 8517.12.00, vishikwambi (Tablets) HS Code 8471.30.00 au 8517.12.00 na Modemu HS Code 8517.62.00 au 8517.69.00.

Alisema serikali imechukua uamuzi huo kwa kuwa msamaha husika haujawezesha kupatikana kwa bidhaa hizo muhimu kwa bei nafuu kwa walengwa na badala yake unawanufaisha wafanyabiashara.

"Hatua hii inalenga kuiongezea serikali mapato kiasi cha Sh. milioni 33,705," alisema.

Serikali pia imependekeza kupanda kwa ushuru wa forodha kwa vifaa vya ujenzi vinavyotumia malighafi kutoka nje ya nchi ili kulinda na kukuza viwanda vya ndani na kuongeza ajira. Vifaa hivyo ni mabomba ya plastiki, mabati, marumaru na aliminium.

Pia imependekeza kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwenye malighafi, vipuri na mashine vinavyotumika katika kutengeneza viatu vya ngozi na nguo kwa lengo la kuhamasisha ukuaji wa sekta ya nguo na viatu vya ngozi nchini.

Serikali imependekeza kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye mabasi ya abiria yanayoingizwa nchini kwa ajili ya mradi wa mabasi yaendayo haraka.

Pia kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 25 kwa 140 mwaka mmoja kwenye matairi mapya ya pikipiki kwa lengo la hatua hii ni kuhamasisha uzalishaji wa matairi hayo nchini kwa kuwa kuna malighafi za kutosha.


**TOZO MIAMALA**

Serikali imependekeza kupunguza tozo ya muamala kutoka kiwango kisichozidi Sh. 7,000 hadi Sh. 4,000 katika kila muamala wa kutuma na kutoa pesa ili kupunguza mzigo kwa wananchi.

"Punguzo hili ni sawa na asilimia 43 ya kiwango cha sasa. Sambamba na hilo, napendekeza kuongeza wigo wa tozo hiyo ili kuhusisha miamala yote ya kielektroniki," alisema Waziri Nchemba.

**KARATASI**

Alisema anapendekeza kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye karatasi zinazozalishwa na viwanda vya nchini na kwamba hatua hiyo inalenga kulinda viwanda vinavyozalisha karatasi hizo nchini.



Rais Samia Suluhu Hassan, akifuatilia kupitia runinga hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka 2022/2023, iliyokuwa ikiwasilishwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, bungeni jijini Dodoma, akiwa Muscat, nchini Oman jana. **PICHA: IKULU**

# Biashara za mtandaoni, ving'amuzi kutozwa kodi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imependekeza kukusanya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye biashara mtandao.

Akiwasilisha jana mapendekezo ya mapato na matumizi ya serikali kwa mwaka wa fedha 2022/23 bungeni, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema serikali inapendekeza kurekebisha Sheria ya VAT Sura ya 148 ili kurahisisha utaratibu wa usajili wa walipakodi wanaotoa huduma za kidijitali bila ya kuwa na makazi nchini.

Alisema hatua hiyo inalenga kwenda sambamba na mwamko wa shughuli za kibiashara duniani zinazofanyika kwa njia ya mtandao ambapo inatarajia kuiongezea serikali mapato ya Sh. bilioni 34.24.

**TOZO SIFURI MAFUTA**

Waziri huyo alisema serikali imependekeza kutoza kwa kiwango cha asilimia sifuri katika bidhaa za mafuta ya kula yanayozalishwa nchini kwa mwaka mmoja ili kuleta unafuu wa bei.

Dk. Mwigulu alisema pia serikali inapendekeza kutoa msamaha wa VAT kwenye miti ambayo haijachakatwa ambapo hatua hiyo itapunguza mapato kwa Sh. bilioni 8.814.

"Kusamehe VAT kwenye malighafi zinazotumika kuzalisha mitungi ya gesi zinazotambulika ili kuwapa unafuu wazalishaji wa mitungi ya gesi na kulinda viwanda vya ndani," alisema.

Aliongeza kuwa msamaha husika utatolewa baada ya mzalishaji kutia saini Mkataba wa Utekelezaji na Serikali.

Pia, alisema anapendekeza kutoza VAT kwa kiwango cha sifuri kwenye mbolea inayozalishwa nchini kwa mwaka mmoja, kutoa VAT kwenye vifaa vya kupima kiwango cha maji na unyevunyevu kwenye udongo ambapo hatua hiyo itapunguza mapato ya serikali ya Sh. bilioni 2.99.

"Kusamehe VAT kwenye vyandarua vinavyotumika katika uzalishaji wa mboga na maua, vifaa vya kupima kiwango cha unyevunyevu, hatua hii inatarajia kupunguza mapato ya serikali kwa kiasi cha Sh. bilioni 1.63," alisema.

Waziri huyo alipendekeza kusamehe VAT kwenye magari yenye jokofu na vyumba vya ubaridi ili kuzuia mazao kuharibika baada ya mavuno na kuchochea kilimo cha kisasa na hatua hiyo inatarajia kupunguza mapato ya serikali kwa Sh. bilioni 3.74.

Pia alisema kusamehe VAT kwenye vanila ya kijani isiyochakatwa, kamba za katani zinazozalishwa nchini, mtindi (yoghurt) na maziwa yanayozalishwa kwa joto la juu na kudumu kwa muda mrefu, vifungashio vya maziwa, hereni za mifugo za kielektroniki, vifaa vya machinjio, mbegu za malisho, vifaa na mitambo ya hali ya hewa vinavyoingizwa

.

**KODI YA ZUIO**

Alipendekeza kuondoa msamaha wa kukata Kodi ya Zuio kwenye malipo ya upangishaji nyumba, vyumba na majengo ya biashara na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato (TRA) ataingia makubaliano ya uwakala na Ofisi ya Rais - TAMISEMI juu ya usimamizi na ukusanyaji wa kodi hiyo.

Dk. Mwigulu pia alipendekeza kutoza kiwango cha mfuto (flat rate) cha Sh. milioni 3.5 ikiwa ni kodi ya mapato inayopaswa kulipwa kwa kila magari ya mizigo na mabasi ya abiria kwa mwaka na hatua hiyo inatarajiwa kuiongezea mapato ya Sh. milioni 141.05.

**MIKOPO MAKUNDI MAALUM**

Alipendekeza kugawanya asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri ambapo asilimia tano ipelekwe kwenye miundombinu na masoko ya machinga, asilimia mbili kwa ajili ya mikopo kwa vijana, asilimia mbili kwa ajili ya wanawake na asilimia mbili kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

**TOZO VING'AMUZI**

Pia alipendekeza kuanzisha utaratibu wa kutoza ada ya Sh. 1,000 hadi 3,000 kwenye ada ya matumizi ya king'amuzi kulingana na kiwango cha matumizi.

## Deni la serikali lapaa kwa 14%

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

DENI la serikali limeongezeka kutoa Sh. trilioni 60.72 Aprili 2021 hadi Sh. trilioni 69.44 Aprili 2022, ikiwa ni ongezeko la asilimia 14.4.

Katika mchanganuo wa ukuaji wake, deni la nje limekua kutoka Sh. trilioni 22.37 hadi 47.07 huku sababu za ongezeko hilo zikitajwa kuwa ni mikopo mipya kutoka vyanzo vyenye masharti nafuu na ya kibiashara kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alibainisha hayo bungeni jijini hapo jana alipowasilisha Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2022/23.

"Ongezeko la deni lilitokana na kutolewa kwa hatifungani maalumu yenye thamani ya Sh. trilioni 2.18 kwa ajili ya deni la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) lililotokana na michango ya watumishi wa kabla ya mwaka 1999.

"Taarifa ya tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Novemba 2021, inaonyesha kuwa deni la serikali bado ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu kwa kuzingatia ukomo wa viashiria vyote vinavyokubalika kimataifa," alisema.

Kuhusu ugharamiaji wa mpango wa 2022/23, alisema serikali inakadiriwa kuwa jumla ya Sh. bilioni 15,004.8, sawa na asilimia 36.2 ya bajeti yote ya serikali zitatumika kugharamia miradi ya maendeleo ikijumuisha miradi ya huduma za jamii.

Dk. Nchemba alisema katika kuongeza ushiriki wa sekta binafsi kama injini muhimu ya utekelezaji wa miradi, serikali itahakikisha miradi yote inayovutia uwekezaji wa sekta binafsi inatekelezwa kwa utaratibu wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) na 'Joint Venture' (ubia) kwa kutumia utaratibu wa kampuni maalumu (Special Purpose Vehicle).

VisionFund TANZANIA MICROFINANCE BANK LTD

# VISIONFUND TANZANIA MICROFINANCE BANK LTD

# VACANCIES

VisionFund Tanzania Microfinance Bank Ltd (VFT MFB) formerly known as SEDA is a fast growing and reputable Micro Finance Bank (MFB), has a loan book of TZs. 17 billion and 30,000 customer base, more that 5,000 of them being small holder farmers. VFT-MFB is seeking to employ a dynamic and committed Tanzanian young men & women who have passion for people's economic development to fill in the vacant positions detailed here below;

**Work reference no.** : **009/22**
**Position** : **Business Centre Manager**
**Reporting to** : **Regional Manager**

**Responsibility:**

- To develop business plan and annual work plan of the Business Centre and ensure an efficient performance of the Business Centre to achieve the set targets. To market VFT-MFB products and services & conduct market survey within the prescribed areas of operation.

**Main tasks**

1. To ensure efficient performance of the Business Centre
2. Ensures that the Business Centre meets or exceeds the targets as agreed upon the business plan
3. Chairs Business Centre Credit Committee and participates in evaluating, approving or rejecting loans according to policies
4. Implements policies, procedures and internal controls at the Business Centre
5. Oversees implementations of internal controls, audit issues and compliance at the Business Centre
6. Mentoring and coaching of staff and maintains a harmonious working relationship among the staff
7. Monitors staff performance and coordinates with P&C on performance management
8. Develop & maintains good working relations with staff, customer relationship and ensure customer satisfaction

**Education/Experience**

- Bachelor Degree in Economics, Marketing, Accounting and Business Administration
- Very good knowledge of oral & written English
- Very good analytical & reporting skills
- Proficient with Microsoft applications
- 3 years' experience Banking or Microfinance operations

**Work reference no.** : **010/22**
**Position** : **Loan Officer**
**Reporting to** : **Branch/Business Centre Manager**

**Responsibility**

- To build and maintain a high quality loan portfolio which involves identifying clients, implementing and managing a credit program within a designated operation area of VFT-MFB and in accordance to the set policy and procedures.

**Main Tasks**

1. Does client recruitment and orientation to VFT-MFB loan products and services.
2. Process loan applications and do follow up on loan repayments.
3. Provide quality and good customer service to clients this include business counselling

**Education/Experience**

- Bachelor Degree in Marketing, Accounting, Business administration and Community Development.

**Special / Personal Abilities**

- Excellent character and unquestionable integrity
- Ability to do exact and detailed analysis for all loan applications
- Good negotiation skills and highly determined to accomplish tasks
- Good Oral and written communication skills
- Have a very clean bill of health willingness to take on field work
- Must be a self-starter, highly motivated, organized, and detail-oriented
- Model and demonstrates effective Christian leadership
- Motor cycle driving license

**Work reference no.** : **011/22**
**Position** : **Call Centre Officer**
**Reporting to** : **Operations Manager**

**Responsibility**

- Call Center Officer is required to ensure maximum customer satisfaction by receiving customer calls and handling customer enquiries on time.

**Main Tasks**

1. To initiate reconciliation process by calling customers from customer suspense account for the customers paid via Mobile operators
2. To record customer inquiries & complains from outgoing calls and respond accordingly or assign responsible parties and follow-up response
3. To collect exit customer feedback and customer satisfaction survey especially for drop-out customers with good repayment history
4. To conduct Disbursement tests before loan and/or after loan disbursement on sampling basis especially for loans above branch level
5. To report suspicious/alarming call findings to supervisor/Head of department.
6. To conduct Delinquency test from CRM portal to establish if true and produce complied report to responsible parties and Management.
7. To prepare weekly/monthly consolidated Customer feedback from outgoing calls, disbursement and delinquency test report for SMT

**Education/Experience**

- Bachelor Degree in Customer Relations, Business Administration, Human Resources or any related field.
- Must have a clear understanding of microfinance bank activities
- Very good knowledge and comfort dealing customers from diverse societies
- Very good analytical & reporting skills
- Proficient with Microsoft applications
- At least 1 (one) year experience in Call Centre operations

**Work reference no.** : **012/22**
**Position** : **Personal Assistant**
**Reporting to** : **Chief Executive Officer**

**Responsibility**

- Provide full administrative and secretarial support to the CEO and ensure smooth management of day to day affairs, and most effective use of his/her time. Handle sensitive and complex issues in a professional and objective manner and take initiatives as appropriate in CEO's absence.

**Main Tasks**

1. To manage CEO's electronic diary and manage his calendar appointments accordingly
2. To manage CEO's travel arrangements for Business and personal activities
3. Ensure all incoming correspondences are dealt with by the CEO or other staff as appropriate
4. Maintain records of CEO's contact, data management and filling
5. Screen calls, inquiries and requests, and deal with them when appropriate
6. Organize meetings and ensure the CEO is well prepared for those meetings, prepare meeting agendas, pre-meeting briefings, meeting papers and minutes preparation
7. Produce documents, briefing papers, reports, presentations for the CEO and proof read all incoming & outgoing documents
8. Prepare CEO's travel expenditure sheet and Per Diem retirements

**Education/Experience**

- Bachelor Degree in Customer relation, Business administration or any related field.
- Exceptional interpersonal and communication skills, Very good knowledge and comfort dealing visitors from diverse societies
- Very good analytical & reporting skills
- Ability to deal with sensitive information with discretion and maintain confidentiality
- Proficient with Microsoft applications
- At least 1 (one) year experience in the position

**Work Reference No.** : **013/22**
**Position** : **Customer Service Officer**
**Reporting to** : **Business Centre Manager**

**Responsibility:**

- Provides support to Business Centre Manager in day to day activities related to data entry in VFT MFB system
- Provide satisfactory customer service to VFT internal and external customers

**Main tasks**

1 Attends customer inquiries
2 Promotes/markets Savings
3 Directs customers to respective officer or right channel
4 Monitors/attends customers' ATM usage
5 Register and solve customers' compliances
6 Pass right information to customers
7 Issues marketing tools such as fliers to customers
8 Ensure accurate data entry
9 Acknowledges bank correspondence
10 Sends disbursement sheet to Central Processing Center
11 Post and receive the Business Centre Parcels
12 Does photo copy and printings
13 Keeps the Business Center stationeries
14 Keeps under safe custody all clients loan collaterals, files, documents and other valuable item
15 Opens savings accounts
16 Petty cash reimbursement/disbursement as per policy
17 Effect cash and cheque payment s as per authorized, approved or request voucher
18 Ensure payment of services delivery agents/partners e.g. bills, contractors, labour wages if any
19 Purchases of office items e.g. water, sugar, utensils e.t.c

**Education & Experience:**

- Bachelor Degree in Accounting,
- Must have a clear understanding of data entry and technology
- Very good knowledge and comfort dealing with financial information
- Very good analytical & reporting skills
- Proficient in Microsoft office application
- Be a good leader
- Very good communication and marketing skills (both written and verbal)

**Mode of Application:**
Interested and suitably qualified individuals should forward their application letter, attaching copies of their academic and professional certificates; detailed CV's with three referees to; **vftHRstaff@vftz.co.tz.**

The position should be the subject of the email application.

OR; through the postal address below:

**The Chief Executive Officer,**
**VisionFund Tanzania Microfinance Bank Limited,**
**P. O. Box 1546,**
**Arusha TANZANIA**.

The application should reach the undersigned not later than
**26th June 2022.**

**N.B. Only short-listed candidates will be contacted**

**Disclaimer**
VisionFund Tanzania Microfinance Bank would like to inform the general public that it has not engaged any consultant/agent to conduct recruitment on its behalf.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Royal Tour itumike kupanua uwekezaji nchini

**WINGI** wa watalii wanaoingia nchini kwa sasa unaonyesha kuchangiwa na matokeo ya filamu ya Royal Tour na kulegezwa kwa masharti ya corona ambayo yamesaidia wageni kusafiri bila vikwazo vigumu.

Programu ya filamu ya Royal Tour ilizinduliwa Aprili, 2022 katika Jiji la New York na Jiji la Los Angeles nchini Marekani na kuendelea katika Jiji la Arusha, Dar es Salaam, Zanzibar na Dodoma.

Katika uzinduzi nchini Marekani, zaidi ya watu 6,000 walishiriki wakiwamo viongozi wa kitaifa wa majiji husika, watu maarufu, wawekezaji, wadau wa utalii na uhifadhi na wafanyabiashara mbalimbali.

Uzinduzi huo pia ulishirikisha vyombo mbalimbali vya habari vya kimataifa vikiwamo; vituo vya televisheni na redio vya CBS, Fox News, NBC, YouTube na PBS - Amazon Prime video.

Kwa mujibu wa Chama cha Waongoza Watalii Tanzania (TATO), mwishoni mwa Machi, mwaka huu, chama hicho kimepokea wageni zaidi ya watalii 300,000 kutoka Ulaya na 50,000 Marekani hali inayofanya hoteli zinazopokea na kulaza wageni kuelemewa.

Tunasema huu ni mwanzo mzuri wa matokeo ya filamu ya Royal Tour kuutangaza utalii wa Tanzania na kufanya watu wa mataifa mengine ya nje kuvutiwa kuja kuona vivutio vyetu.

Fursa hii itumike kuwekeza kwenye hoteli nyingi zaidi zitakazoweza kupokea wageni badala ya kuwapoteza kwa kukosa pa kuwaweka.

Pia wageni wa mataifa mengine kama Ufaransa, Italia, Dubai, Uturuki pamoja na Spain, wameanza kuingia nchini kwa wingi kushuhudia vivutio hivyo.

Kiuchumi, maliasili na malikale zimeendelea kuchangia katika kuingiza fedha za kigeni na Pato la Taifa (GDP) kupitia utalii, ajira, nishati, elimu, utafiti, utamaduni, burudani na tiba. Sekta ya Utalii huchangia takribani asilimia 25 ya fedha za kigeni na zaidi ya asilimia 17 katika Pato la Taifa.

Kutokana na juhudi za serikali za kuendeleza na kuimarisha utangazaji wa vivutio vya utalii nchini, idadi ya watalii wanaoingia nchini kutoka katika nchi mbalimbali duniani imeongezeka kutoka 9,847 mwaka 1960 hadi kufikia watalii 1,527,230 mwaka 2019. Kadhalika, kumekuwapo na ongezeko la mapato yatokanayo na watalii, kwa mfano mwaka 1995 mapato yalikuwa Dola za Marekani milioni 259.44 na yaliendelea kuongezeka hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 2.6 mwaka 2019 kabla ya ugonjwa wa UVIKO-19.

Kutokana na serikali kukabiliana na ugonjwa wa UVIKO-19 idadi ya watalii imeanza kuongezeka kutoka watalii 620.867 mwaka 2020 hadi kufikia 716,169 Oktoba 2021.

Juni 4, mwaka huu, kwa mara ya kwanza kampuni ya watalii duniani ya Eurowings Discovery ilitua katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), ikiwa na watalii 130 waliokuja kutembelea vivutio mbalimbali kama Mlima Kilimanjaro, Zanzibar, Serengeti na Ngorongoro.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alisema kuja kwa ndege hiyo ni heshima na jambo muhimu kwa sekta ya utalii, huku Mwenyekiti wa Bodi ya KADCO, Dk. Natu Mwamba, akisema filamu hiyo imeongeza ujio wa watalii na wawekezaji nchini.


Wiki iliyopita, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alilieleza Bunge kuwa kwa sasa kuna mafuriko ya watalii huku akisema mji wa Karatu umepokea wageni wengi kuliko miaka mingine na kichocheo kikubwa ni filamu ya Royal Tour.

Wizara ya Maliasili pia imeendelea kuhamasisha utalii wa ndani kupitia kampeni na programu mbalimbali, hatua ambazo zimeongeza idadi ya watalii wa ndani waliotembelea maeneo ya hifadhi, vituo vya malikale na makumbusho kutoka watalii 562,549 mwaka 2020 hadi 788,933 mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 40.2. Ongezeko la idadi ya watalii limechangiwa na juhudi mbalimbali zikiwamo; kampeni za kutangaza utalii, maadhimisho na maonyesho mbalimbali.

Uhamasishaji huu uwe chachu pia ya kuboresha vituo vingi zaidi na kuvutia watalii wengi kuvitembelea.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wananchi wasimamie miradi si kusubiri Mwenge

Na Sabato Kasika

**MIRADI** 52 ya maendeleo katika mikoa mbalimbali ilikataliwa wakati wa mbio za Mwenge wa Uhuru za mwaka jana, kutokana na kile kilichoelezwa kuwa ni kujengwa chini ya kiwango.

Hiyo ni taarifa ilitolewa na Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, wakati akizindua mbio za Mwenge mwaka huu wa 2022 mjini Njombe.

Kutokana na hali hiyo, akawaagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kuharakisha uchunguzi, ili watuhumiwa wa kuchakachua kazi za ujenzi na miradi mingine wafikishwe mahakamani haraka na haki itendeke.

Kuchakachua miradi ya maendeleo, ufisadi na hata wahusika kutofanya kazi za kandarasi wanazopewa imekuwa ikiibuliwa na Mbio za Mwenge wa Uhuru kila mwaka, hali ambayo inaonyesha kuwa huenda wananchi hawajui wajibu wao na haki ya kufuatilia utekelezaji wa miradi katika maeneo yao.

Ikumbukwe kuwa, serikali imekuwa ikitafuta fedha hata za mikopo nje na ndani ya nchi na nyingine pesa zinazotolewa na walipa kodi ili kujenga miradi mbalimbali ya maendeleo kwa ajili ya wananchi wake, hivyo hujuma zinazoibuliwa na Makamu wa Rais, zinaongeza uchungu.

Hivyo, wananchi kwa upande wao ni vyema sasa wakaamka na kujua kuwa ni nguzo muhimu ya kufuatilia na kuhakikisha miradi hiyo inalingana na thamani ya fedha iliyotumika badala ya kujiweka pembeni na kuacha wajanja wachache wajinufaisha kwa jasho la Watanzania wengi wakiwamo maskini wanaovuja jasho.

Ingependeza kuona kuwa wananchi wanashirikishwa na wanafuatilia kwa karibu utekelezaji wa miradi ili kodi ambayo wanaitoa iwe na matokeo chanya.

Watanzania iwe kijijini au mjini kwenye mradi wa umeme, maji, hospitali, shule au barabara kukaa kimya hadi uchakachuaji uibuliwe na Mwenge wa Uhuru, ni sawa na kuruhusu hujuma hizo ziendelee kuwapo bila kudhibitiwa.

**Kwa mfano, daraja linaweza kujengwa chini ya kiwango na baadaye likabomoka na likasababisha maafa kwa watumiaji.**

Hujuma hizo zinaweza kusababisha serikali isifikie ilichokusudia kukifanya kwa ajili ya maendeleo hayo ya nchi na watu wake.

Uchakachuaji wa miradi ya maendeleo unaoongeza gharama zisizotarajiwa kwa kurudia upya ujenzi wa wake lakini pia kutumia fedha mara dufu.

Ninadhani kwamba, Mbio za Mwenge wa Uhuru za mwaka huu zisaidie kuwakumbusha wananchi kufuatilia miradi inayotekelezwa katika maeneo yao na kuondolea dhana kwamba ufuatiliaji huo ni jukumu la serikali.

Pia ninaamini kuwa serikali inapotoa fedha kwa ajili ya maendeleo inatarajia kuona zinatumika ilivyokusudia, ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa miradi kulingana na thamani ya fedha iliyotumika.

Jambo hilo linahitaji usimamizi na ufuatiliaji wa pamoja kuanzia kwa wananchi na serikali, ili kuziba mianya yote ya uchakachuaji ambayo imekuwa ikitumiwa na baadhi ya wasimamizi.

Kimsingi, wasimamizi hawapaswi kutumia nafasi za kujinufaisha kwa kodi za Watanzania na kutekeleza miradi chini ya kiwango, jambo ambalo ni hatari, lakini ni kukosa hofu ya Mungu na hata kusababisha hatari na kutishia maisha.

Kwa mfano, daraja linaweza kujengwa chini ya kiwango na baadaye likabomoka na likasababisha maafa kwa watumiaji.

Hivyo, ni vyema wananchi wawe mstari wa mbele kufuatilia miradi inayotekelezwa kwenye maeneo yao, kwa ajili ya maendeleo, lakini na usalama wao.

Utaratibu huo unaweza kusaidia kuziba mianya ya hujuma inayotumika kutekeleza miradi ya maendeleo chini ya kiwango na kuisababishia serikali hasara na kuongeza umaskini kwa taifa.

Viongozi wa CCM, serikali, vyama vya upinzani na asasi za kiraia washiriki kufuatilia na kupigia kelele kazi hafifu kwenye maeneo yao na kuiarifu TAKUKURU badala ya kusubiri Mwenge.

Heri kukinga ufisadi kuliko kuuacha ufanikiwe.

## WFP yatumia bil. 5/- miradi ya wakulima

**Na Faustine Feliciane,** KIGOMA

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), limetumia zaidi ya Shilingi bilioni tano kutekeleza mradi wa kuwainua wakulima katika wilaya za Kasulu, Kibondo na Kakonko.

WFP Kwa kushirikiana na mashirika mengine ya Umoja wa Mataifa wanatekeleza mradi wa 'Kigoma Joint Program' (KJP) na WFP imejikita kwenye sekta ya kilimo na kutumia kiasi hicho cha fedha kutekeleza mradi huo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkuu wa Ofisi ya WFP wilayani humo, Said Johari, alisema kuwa mwanzo wa mradi huo ulioanza mwaka 2018, WFP imetumia Sh. milioni 137 kukarabati maghala ya kuhifadhia mazao ambayo yalikuwa katika hali mbaya na hayakuwa yakitumika.

"Milioni 137 pekee zimetumika kwenye kukarabati maghala hayo, Kasulu yapo zaidi ya matatu, Kibondo mawili, pia tumenunua maturubai, vifaa vya kupima unyevunyevu kwenye mazao," alisema Johari.

Alisema, wametumia Sh. milioni 237 kutengeneza maeneo ya kukaushia mazao katika wilaya tatu, pia Sh. milioni 84 kununua vifaa zikiwamo mashine 26 za kupukuchulia mahindi.

"Mashine hizi zimegawanywa katika wilaya nne, Kasulu DC mashine saba, Kasulu (3), Kibondo (9) na Kakonko (7) ambazo zote zimekabidhiwa kwa wakulima kupitia Amcos zao," alisema Johari.

"Fedha bilioni 4.5 zimetumika kwenye utekekezaji wa miradi mbalimbali na hizi nyingine jumla yake milioni 596 zimetumika kwenye ununuaji wa vifaa na ukarabati niliousema, jumla yake sasa fedha zilizotekekeza mradi zinafika bilioni 5.96," alisema.

Aidha, Kwa msimu huu wa mazao, WFP imepanga kununua tani 43,000 nchi nzima kwa ajili ya kulisha wakimbizi wa ndani na nje ya nchi.

"Tumepanga kununua tani 3,000 za maharagwe, 10,000 za mtama na 30,000 za mahindi, mazao haya hususani mahindi na maharagwe tunategemea kupata kwa wingi hapa Kigoma, lakini pia tutanunua na mikoa mingine," alisema Johari.

Mkuu wa Wilaya ya Kibondo, Kanali Aggrey Magwanza, alisema mradi huo wa KJP, WFP wamefanya mambo makubwa katika kuwainua wakulima kwa kuweka mazingira mazuri katika kilimo.

"WFP wametusaidia sana kwenye soko la mazao ya kilimo, kwa sasa wakulima wa hapa Kibondo, Kasulu na Kakonko hawana hofu ya soko la mazao yao, wenzetu hawa wananunua mazao yote yenye ubora hususani mahindi na maharagwe," alisema Kanali Magwanza.

Alisema kutokana na elimu kwa wakulima na uwekezaji wa WFP, soko linazidi kupaa ikilinganishwa na hali ilivyokuwa kabla ya kuwapo kwa mradi huo wa KJP.

"Huko nyuma mkulima alikuwa hanufaiki, mtu wa kati (dalali) ndiye alikuwa ananufaika zaidi, lakini tangu WFP waingie sokoni kununua mazao, mkulima anaona thamani ya jasho lake," alisema Kanali Magwanza.

# NEMC yafanya ukaguzi SGR

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Wakurugenzi wa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) imefanya ukaguzi katika mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) na kushauri masuala mbalimbali ya mazingira.

Hatua hiyo ya NEMC ni utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge, Uwekezaji, Viwanda na Mazingira ambapo waliagiza miradi ya kimkakati inapojengwa baraza hilo lifuatilie kwa karibu badala ya kusubiri athari zitokee ndio hatua zichukuliwe.

Akizungumza jana katika ziara hiyo ya ukaguzi kutoka Dar es Salaam hadi Ruvu, Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Prof. Esnath Chaggu, alisema wamefika kukagua uzingatiaji wa masuala ya mazingira katika mradi huo mkubwa wa muhimu kwa taifa.

"Usafirishaji kwenye nchi yetu ni suala la muhimu sana ndiyo maana mradi huu mkubwa umeanzishwa, kwa taarifa ambazo tumezipata uzingatiaji wa masuala ya mazingira unafanyika vizuri sana na wanafuatilia kwa karibu," alisema.

Aliongeza kuwa Shirika la Reli Tanzania (TRC) limeamua kuanzisha kitengo maalum kinachohusika na mazingira ambapo wanahakikisha wameajiri wataalamu wa mazingira.

Mwenyekiti huyo alisema utendaji kazi ukiwa na wataalamu ni jambo jema na kitengo hicho ni muhimu kuwapo kwenye shirika hilo.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema ziara ni utekelezaji wa kamati hiyo ili kutosubiri athari zitokee ndipo baraza lichukue hatua.

"Hata Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akisisitiza miradi hii mikubwa ya maendeleo sisi NEMC tuwe karibu nayo ili kushauri pale mambo hayaendi vizuri ya kimazingira," alisema.

Alibainisha kuwa katika ziara hiyo wamezungumza na menejimenti ya TRC ambapo miongoni mwa mambo yaliyozungumzwa ni kero ambayo wananchi wamekuwa wakiipata wakati wa ujenzi ikiwamo eneo la Kipawa kuwa na mafuriko.

"Tumeshauriana jinsi ya kuchukua hatua ili kusitokee tena tatizo, kuna maeneo mbalimbali kwenye hii SGR walikuwa wamezoea kuyavuka, sehemu kubwa sasa hawataweza kuvuka kutokana na senyenge kubwa ambayo imewekwa kwa usalama wao, maeneo hayo tumeshauri," alisema.

Alieleza kuwa menejimenti hiyo imesema mipango ipo mbioni ya kuondoa kero kwa wananchi hasa ya vivuko kwa watu wanaokwenda kwa miguu.

"Pale Majumba Sita na maeneo mengine wameanza ujenzi wa vivuko, tunataka reli hii iwe rafiki kwa watu," alisema.




Ofisa Huduma kwa Wateja wa Benki ya NMB, Neema Kazoviyo (katikati), akibonyeza kompyuta kuwasiliana na mmoja wa washindi 10 wa droo ya Bonge la Mpango Awamu ya Tatu, chini ya kampeni ya Teleza Kidijitali ya NMB, katika tawi la benki hiyo, Gongolamboto, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mwakilishi wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), Irene Kawili na Meneja wa tawi hilo, Demetrius Kugesha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## RC Homera aipongeza TARI maonyesho kilimo biashara

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ameipongeza Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kwa kuandaa maonyesho ya kilimo biashara katika mashamba ya mfano ya TARI Uyole kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa kilimo likiwamo Baraza la Nafaka la Afrika Mashariki (EAGC).

Katika hotuba yake wakati akifungua maonyesho hayo, Homera aliwataka wakulima na wadau wa kilimo kuzingatia kanuni bora za kilimo kwa kutumia mbegu bora na kushirikiana na wataalamu wa kilimo ili kupata utaalamu wa uzalishaji wa mazao yenye tija katika kuinua uchumi wa nchi.

Alizitaka taasisi za huduma za kilimo ukiwamo Wakala wa Pembejeo (mbolea, mbegu bora na viuatilifu) kuweka programu endelevu za upatikanaji wa pembejeo hizo na kuwataka wataalamu wa kilimo kuendelea kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mbegu bora, mbolea na viuatilifu kwa wakulima ili kuongezea tija.

Maonyesho hayo yaliyobeba kaulimbiu 'Mageuzi ya Kilimo Biashara, Jiandae Kuhesabiwa kwa Mipango Endelevu', ni sehemu ya utekelezaji wa

Agenda 10/30 inayoongozwa na kaulimbiu ya 'Kilimo Biashara'.

Akitoa salamu za TARI katika maonyesho hayo, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu, Dk. Richard Kasuga, alimshukuru mgeni rasmi na uongozi wa Mkoa wa Mbeya kwa kuweka kipaumbele kusaidia utafiti hususan Kituo cha TARI Uyole.

Dk. Kasuga pia aliipongeza na kuishukuru serikali na Wizara ya Kilimo Bashe kwa kutenga fedha kwa ajili ya utafiti na kuzalisha mbegu bora ili kuongeza tija, kuwa na uhakika wa chakula, kipato, kuboresha lishe na kuchangia ukuaji wa uchumi katika nchi.

Dk. Kasuga alisema katika mwaka 2021/22, serikali ilitenga TARI Sh. bilioni 11 kwa ajili ya maendeleo kutoka takribani Sh. bilioni saba mwaka 2020/21 na katika mwaka 2022/23, serikali imeitengea TARI Sh. bilioni 41 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambayo itachangia ufikiwaji wa Agenda 10/30 kwa kuongeza upatikanaji wa mbegu bora na kuendeleza utafiti wa kilimo nchini.

Mkurugenzi wa Kituo cha TARI Uyole Dk. Tulole Bucheyeki, alisema maonyesho haya ya kilimo biashara ambayo yanafanyika kwa mwaka wa nne mfululizo, yamekuwa na mafanikio makubwa kwa kuwaunganisha wadau wa kilimo katika mnyororo wa thamani. Dk. Bucheyeki aliongeza kuwa matokeo ya utafiti hayawezi kuleta tija inayokusudiwa bila kushirikisha wadau wa kilimo katika kuzisambaza teknolojia hizo ili zilete matokeo tarajiwa.

Katika maonyesho ya kilimo biashara, TARI ilitambulisha teknolojia za mazao ya nafaka (ngano, mahindi na ulezi), maharage, soya, pareto, viazi mviringo, parachichi na uhandisi kilimo.

Taasisi na kampuni zingine zilizoshiriki maonyesho ya kilimo biashara ni Seed Co, Kibo Seed, Highland Seed Growers, Beula Seed, Agriseed, Mashamba and Tractor, Syngenta Tanzania, Agro Z na Mosanto.

Zingie ni YARA, Minjingu, Zam seed, Meru Agro, CORTEVA, MATI Uyole, TALIRI, Western Seed na PANNAR.

# Wanajeshi warejea na mikakati kuukabili ugaidi

**Na Richard Makore,**
MWANZA

KIKOSI cha askari wa ulinzi na usalama cha watu 293 kilichoenda kwenye mafunzo maalum yaliyohusisha nchi sita za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), kimerejea nchini kikiwa na mambo makuu manne.

Kikosi hicho kilichorejea juzi nchini na kufikia jijini Mwanza kimekuja na mikakati maalumu ya kuzuia na kupambana na suala a ugaidi nchini.

Katika kutekeleza suala hilo, kikosi hicho ambacho kimekaa nchini Uganda kwa siku 14, kimejifunza mbinu mbalimbali za kukabiliana na tatizo la ugaidi.

Aidha, kikosi hicho kimerejea kikiwa na mkakati wa kukabiliana na majanga, uharamia na kulinda amani kwa hapa nchini pamoja na nchi za (EAC).

Wapiganaji hao pamoja na raia jana walikabidhi bendera ya taifa waliyokabidhiwa na Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Nchi Kavu, Meja Jenerali, Antony Sibiti wakati wanaondoka katika kikosi cha usafirishaji cha Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), kilichopo Nyegezi, mkoani Mwanza, Mei 28, mwaka huu.

Akizungumza na askari hao jana jijini hapa, Meja Jenerali Sibiti, alisema kikosi hicho kimerejea kikiwa na mafunzo yaliyokusudiwa.

Alisema kimejifunza masuala ya kupambana na ugaidi, uharamia, kulinda amani na majanga mbalimbali yanapotokea kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Alisema lengo la mafunzo hayo ambayo yalijulikana kama ushirikiano imara, yalilenga kupata mbinu za kupambana na ugaidi katika nchi wanachama wa EAC, kusaidia nchi inayokumbwa na machafuko ya kisiasa (kulinda amani), kupata mbinu za kukabiliana na maafa ama majanga pamoja na uharamia.

Aliwataka askari hao kutumia mafunzo waliyoyapata nchini Uganda kulinda nchi yao na kuwa wazalendo wa kweli.



Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo (kulia), akikabidhi moja ya pikipiki tano aina ya Hero Hunter 125cc kwa Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, ACP Muliro Jumanne Muliro, zilizotolewa msaada na Kampuni ya Hero Motorcorp, kwa ajili ya matumizi ya jeshi hilo, jijini jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadau wilaya 12 wapatiwa elimu kuhusu sumukuvu

**Na Joseph Mwendapole**

WADAU kwenye mnyororo wa mazao ya karanga na mahindi katika wilaya 12 kati ya 18 nchini, wamepatiwa elimu namna ya kukabiliana na tatizo la uchafuzi wa sumukuvu kwenye mazao.

Elimu hiyo inatolewa kwenye wilaya 18 katika mikoa 10 ya Tanzania Bara ambayo ni Dodoma, Morogoro, Mtwara, Ruvuma, Tabora, Mwanza, Simiyu, Geita na Kigoma kutokana na utafiti kuonesha kuwa wilaya hizo zinazozalisha mazao hayo kwa wingi zina tatizo la uchafuzi wa sumukuvu kwa kiwango kikubwa.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Ofisa Viwango wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Mratibu wa Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu Tanzania (TANIPAC) upande wa shirika hilo, Ally Kingazi, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema kuna changamoto mbalimbali zinazochangia tatizo la uchafuzi wa sumukuvu na hutokea wakati wa kuandaa shamba, kuvuna, baada ya kuvuna wakati wa ukaushaji, usindikaji na usafirishaji.

Pia, changamoto nyingine ni kwenye uhifadhi, ambao huchangia uchafuzi wa sumukuvu.

Alisema, serikali kupitia TBS imechukua hatua mbalimbali kwa ajili ya kudhibiti tatizo hilo, moja likiwa ni kutoa elimu, kujengea jamii uelewa wa tatizo hilo na namna ya kudhibiti.

Kingazi alisema shirika limeandaa miongozo mbalimbali ya namna ya kudhibiti sumukuvu.

Alisema mradi huo ni wa serikali ambao unatekelezwa kwa kupitia Wizara ya Kilimo ukiwa na lengo la kuimarisha usalama wa chakula, lishe, pato la mkulima pamoja na taifa kwa ujumla kwa kudhibiti uchafuzi wa sumukuvu kwenye mazao ya mahindi na karanga.

TBS kutokana na jukumu lake la kisheria la kusimamia ubora na usalama wa chakula, linatekeleza moja ya sehemu ya mradi huo kwa kutoa elimu ya sumukuvu kwa wananchi walipo eneo la mradi kwa mazao ya mahindi na karanga.

Alisema lengo kuu la mradi ni kutoa elimu ya sumukuvu ni kujengea uelewa jamii tatizo hilo na namna ya kudhibiti. Aliongeza kwamba sumukuvu ina madhara tofauti katika nyanja za kiafya na kiuchumi.

Kwa upande wa kiafya, Kingazi alisema kuna madhara yanayojitokeza baada ya muda mfupi ni kifo, lakini pia yapo ya muda mrefu mfano saratani ya ini.

## ‘Wazee, wasio makazi wakumbukwe sensa’

**Na Sabato Kasika**

JAMII imetakiwa kukumbuka makundi ya wazee na watu wasio na makazi wakati wa sensa ili nao wahesabiwe, wajulikane idadi na kuingizwa kwenye mipango ya maendeleo ya taifa.

Wito huo ulitolewa jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki na Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Kupinga Ukatili kwa Wazee Duniani.

Alisema, kilele cha maadhimisho ya siku hiyo hufanyika Juni 15 ya kila mwaka, na mwaka huu yana kaulimbiu: “Tuhakikishe wazee wanalindwa, wanasikilizwa na kuheshimiwa, tusikose kuhesabiwa kwenye Sensa ya Watu na Makazi’.

“Ni kupitia takwimu za sensa pekee, ndizo zitaweza kusaidia kupanga mipango mizuri ya nchi, hivyo tunapokwenda kuadhimisha siku hii tusiache wazee na watu wasio na makazi,” alisema Dk. Gwajima.

Waziri Gwajima alisema, ni imani yake kwamba, kila mmoja kwa nafasi yake atakuwa mstari wa mbele kuhimiza zoezi la sensa kwa makundi yote likiwamo la wazee ili kusaidia serikali kupanga mipango ya maendeleo.

“Lengo la maadhimisho hayo ni kuelimisha jamii kuhusu kupinga ukatili wa aina zote dhidi ya wazee ukiwamo wa kimwili, kihisia na kiuchumi, inatakiwa kuelimisha jamii juu ya changamoto zinazowakabili hasa zile zinazotokana na mila na desturi potofu, fursa walizonazo na masuala ya uzee na kuzeeka,” alisema.

Aidha, alitoa takwimu za Jeshi la Polisi kuwa, katika kipindi cha Januari hadi Desemba, mwaka 2020 kulikuwa na matukio 54 ya kuuawa kwa wazee nchini, huku Januari hadi Desemba mwaka jana kukiwa shwari.

“Lakini kipindi cha Januari hadi Juni mwaka huu, takwimu hizo zinaonyesha kuwa kumetokea matukio katika Mkoa wa Singida, Wilaya ya Iramba la mauaji ya wazee watatu wanawake kwa kuhusishwa na imani za kishirikina. Hilo halikubaliki,” alisema.

Aliongeza kuwa, katika kukabilina na tatizo hilo, serikali imeunda mabaraza ya wazee kuanzia ngazi ya kijiji hadi taifa, na kwamba yapo takribani 20,749, mabaraza hayo kwa kushirikiana na wadau yanatumika kutoa elimu kuhusu ukatili dhidi ya wazee.

Katika hatua nyingine, ameitaka jamii kuendelea kujiunga kwenye kampeni ya Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii (SMAUJATA) kupitia kiungio cha https://forms.gle/DtGthrUTLhXJp2cUA pia kwenye mtandao wa kijamii wa Telegram kwa link; https://t.me/+IFypK6_FB-k30TIk. Kwa upande wa Instagram ni @smaujata.tz.

## Mafia yapewa jukumu kuongeza mapato zaidi

**Na Julieth Mkireri,** MAFIA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, amewaelekeza viongozi wa Halmashauri ya Mafia kupanga mikakati mipya ya kuongeza mapato na kukuza uchumi.

Alitoa maelekezo hayo juzi wakati wa Kikao Maalumu cha Baraza la Madiwani cha kujadili taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kilichofanyika wilayani Mafia.

"Kupata hati safi ni kwa mujibu wa hesabu mlizotayarisha, kinachosaidia wananchi pamoja na kupata hati safi ni uwezo wa kifedha wa halmashauri," alisema Kunenge.

Alisema kwa sasa serikali imetoa miradi mikubwa ya kimkakati kwenye halmashauri na kutaka kuibua vyanzo vipya ili waweze kujiendesha.

"Nione zaidi mikakati mipya ya kuongeza mapato kama mipango ni ile ile bajeti ni ile ile hatuwezi kuwa na matokeo mapya kwa kuwa bajeti ni mipango unayoipa gharama," alisema Kunenge.

Alielekeza madiwani wa Halmashauri ya Mafia kupatiwa mafunzo ya uchumi ili waweze kuwa wabunifu wa kuibua vyanzo vipya vya mapato na kutumia fursa za uchumi na uwekezaji katika halmashauri hiyo.

Aliipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Mafia kwa kupata hati safi kwa miaka sita mfululizo.

Kuhusu migogoro ya ardhi kwenye halmashauri hiyo, Kunenge alisema kuwa ameombea fedha serikalini ili kisiwa hicho kipimwe na kupangwa.

Aliwataka viongozi wa halmashauri hiyo kuandaa wananchi na mabadiliko makubwa ya kiuchumi kisiwani humo.

Alimwelekeza Katibu Tawala mkoa kufuatilia hoja zote zilizojirudia na kuwachukulia hatua wote waliosababisha hoja hizo, pia ameitaka halmashauri hiyo kufunga hoja zote zilizo ndani ya uwezo wao ifakapo Septemba 30.

Kuhusu kikwazo cha madaktari na wahudumu wa afya alimwelekeza Mganga Mkuu wa wilaya hiyo kuanza mpango wa hospitali inayotembea (mobile clinic) wakati serikali inatafutia ufumbuzi kikwazo hicho.

Naye Mkaguzi wa Nje wa Hesabu za Serikali, Mary Dibogo, alisema halmashauri hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/21 imepata hati safi na hoja zilizotakiwa kujibiwa ni 54 zilizojibiwa 24 na kubaki 30.

# Zanzibar, Oman kushirikiana katika sekta ya mafuta, gesi

**Na Frank Monyo**

JUMUIYA ya Watoa Huduma katika Sekta ya Mafuta na Gesi (ATOGS) na Jumuiya ya Watoa Huduma katika Sekta ya Mafuta na Gesi Zanzibar, wamesaini makubaliano ya kushirikiana katika sekta ya mafuta na gesi na Jumuiya ya Huduma za Petroli ya nchini Oman.

Makubaliano hayo yamefanyika wakati wa ziara ya kiserikali ya Rais Samia Suluhu Hassan katika nchi hiyo.

Hafla ya kutiliana saini ilifanyika juzi Muscat, wakati wa kongamano la kibiashara huku yakishuhudiwa na Waziri wa Biashara na Viwanda na Uwekezaji wa Oman, Qais bin Mohammed Al Yousef, Balozi wa Tanzania Oman, Abasi Kilima na wawakilishi wa serikali za Oman na Tanzania.

ATOGS iliwakilishwa na Mwenyekiti wake Abdulsamad Abdulrahim na ZAOGS iliwakilishwa na Ali Amour ambaye ni mjumbe wa bodi.

Akiongea na Nipashe muda mfupi baada ya kutiliana saini mkataba huo, Mwenyekiti wa ATOGS, Abdulrahim, alisema utawezesha taasisi hizo tatu uzoefu kwenye maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kipaumbele kwa wazawa pamoja na fursa zilizopo kwenye sekta ya mafuta na gesi kupitia miradi mbalimbali.

"Makubaliano tuliyosaini leo yatawezesha taasisi zetu kuandaa makongamano, warsha na semina za pamoja kwa ajili ya kuwajengea uwezo wanachama wake," alisema Abdulrahim.

Alisema mkataba huo umesainiwa katika muda muafaka. "Ni juzi tu nchi yetu imesaini mkataba wa uchakataji na usindikaji wa gesi asilia na kwa hiyo uzoefu tutakaoupata katika ushirikiano wetu huu utatuwezesha tujipange vyema zaidi kwenye fursa," alisema.

Abdulrahim, aliongeza kuwa OPAL wapo mbele na kwamba watajifunza na kunufaika na mengi kutoka kwao.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Watoa Huduma katika Sekya ya Mafuta na Gesi Tanzania (ATOGS), Abdulsamad Abdulrahim (katikati), Mjumbe wa Bodi ya Jumuiya ya Watoa Huduma katika Sekta ya Mafuta na Gesi Zanzibar (ZAOGS), Ali Amour (kushoto), pamoja na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Jumuiya ya Huduma za Petroli Oman, Abdulrahman Alyahyai, wakisaini mkataba wa ushirikiano kati ya taasisi hizo tatu kwenye sekta ya mafuta na gesi, Muscat, nchini Oman jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# W'biashara wajipanga kutumia fursa kilimo

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

JUMUIYA ya wafanyabiashara mkoani Kagera imejipanga kutumia fursa za kilimo, miundombinu na elimu zilizotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan, wakati akiwa katika ziara ya kikazi ya siku tatu mkoani humo.

Wakizungumza na Nipashe jana, wafanyabiashara hao, Edmund Rusekwa, Jesca Barongo na Richard Maganga walisema kuwa kwa miaka zaidi ya mitano mji wa Bukoba hauna stendi wala soko kubwa ambalo wakazi wangeweza kujivunia kuleta wageni toka nje ya mkoa.

"Tukianzia hapa sokoni hili soko halina mwingiliano namaanisha hakuna watu kutoka mikoa mingine kuja hapa kufanya biashara kama sehemu ya kujipanua kwa uchumi wa mkoa," alisema Rusekwa.

Alisema, miundombinu ya stendi ambayo ingeweza kuleta ongezeko la uchumi kama ingejengwa kisasa ni fursa kwa wafanyabiashara kuwekeza miradi ndani ya eneo hilo, haipo.

Mfanyabiashara wa mazao mjini Bukoba, Richard Maganga alisema, Mkoa wa Kagera una fursa ya ardhi ya kilimo endapo wananchi watajipanga kwa ushirikiano wa viongozi kupitia uzalishaji uchumi utaongezeka.

"Mkoa wetu hauwezi kuwa wa kiwango cha chini katika uchumi zipo ardhi ambazo hazitumiki kwa kilimo, wananchi wakipewa hamasa ya kipi cha kufanya au watumie kulima, umaskini tutasahu," alisema Maganga.

Mhamasishaji na mratibu wa wafanyabiashara mjini Bukoba, Jesca Barongo, alisema jambo linalofanya wafanyabiashara mkoani Kagera kutojipanua na kukuza uchumi ni uwezeshwaji ambao unafikia fursa maeneo yote.

"Mkoa wetu umebarikiwa upo katika mipaka ya nchi ya Uganda, Rwanda, Burundi mipaka ingetosha sisi kuitumia kufanya uchumi na kuondokana na hali ya kiwango cha kusomeka wa chini," alisema.

Aidha alisema, mategemeo yaliyoko baada ya kuondolewa huduma ya malipo ya kodi iliyokuwa ikidaiwa na halmashauri, na kutolewa tamko ianzie mwaka mmoja wa malipo itaweka urahisi wa kufanya jambo la maendeleo ya biashara.

"Alichotufanyia sasa kiongozi wetu wa nchi kuondoa madai ya kuanzia miaka mitatu nyumba na kutaka kuanzia mwaka mmoja kuendelea ilikuwa unakuta mfanyabiashara anadaiwa mwaka 2018, 2019, hadi 2021 na yote yanapigiwa thamani ya malipo," alisema Barongo.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara mkoani Kagera Nicolus Bashwekwa, alisema ustawi wa uchumi wa Kagera unategemea wafanyabiashara ambao wataona fursa za kilimo, elimu na uvuvi.

Alisema, zipo rasilimali nyingi ambazo zikifunguliwa kuwa fursa kama jinsi mkoa ulivyo na mipaka ya mikakati ya kukuza uchumi.

# Wizara Fedha kukabiliana na athari za kiuchumi

WIZARA ya Fedha na Mipango, inaendelea na tathmini ya hatua mbalimbali zinazopaswa kuchukuliwa kwa kila sekta ili kukabiliana na athari za kiuchumi na kijamii zinazotokana na hali ya kisiasa duniani ikiwamo vita ya Russia na Ukraine.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande, alibainisha hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Nancy Nyalusi.

Katika swali lake, Nyalusi alitaka kujua serikali inachukua hatua gani za kukabiliana na athari mbalimbali za kiuchumi zinazotokana na hali ya kisiasa duniani.

Akijibu swali hilo, alisema serikali inafuatilia kwa karibu athari na fursa hizo na hadi sasa imechukuliwa kudhibiti hali hiyo ikiwamo kutoa ruzuku ya Sh. bilioni 100 kwa ajili ya kupunguza bei ya mafuta kwa kipindi cha kuanzia Juni 1, mwaka 2022.

"Hatua nyingine ni kuruhusu wafanyabiashara wenye uwezo wa kuleta mafuta kwa bei nafuu ili kuhakikisha uwepo wa mafuta nchini ambapo mpango huu unatarajiwa kupunguza bei ya mafuta kuanzia mwezi Agosti 2022," alisema.

Kadhalika, alisema kuhamasisha wafanyabiashara kuagiza ngano kutoka nchi nyingine zinazozalisha ikiwamo Afrika Kusini, Canada, Australia, Uswisi na Ujerumani, kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya kuzalisha mbolea nchini kutokana na uhamasishaji huo, kampuni ya Itracom Fertilizers Limited kutoka Burundi inaendelea na ujenzi wa kiwanda mkoani Dodoma na kitakapokamilika kinatarajiwa kuzalisha tani 500,000 kwa mwaka.

"Hatua nyingine ni kuendelea kutekeleza mikakati mahususi ya kukuza utalii wa ndani na kikanda kupitia fursa za Jumuiya ya Afrika Mashariki-EAC, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika-SADC pamoja na Kamisheni ya Utalii ya Shirika la Utalii Duniani kwa Kanda ya Afrika-UNWTO-CAF na kuimarisha sekta ya uzalishaji ikiwamo kilimo cha umwagiliaji," alisema.



Mbunge wa Jimbo la Nyamagana, Stanslaus Mabula, akiuliza swali kwenye kipindi cha maswali, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mbadala uchenjuaji zebaki wapatikana

BUNGE limeelezwa kuwa Wizara ya Madini kupitia mradi wa Environmental Health and Pollution Management Program (EHPMP) imetafuta njia mbadala ya uchenjuaji wa dhahabu ili kuondokana na kemikali ya zebaki.

Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Lupa (CCM), Masache Kasaka.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji hatua za serikali kuhakikisha utaratibu wa kupata baruti na zebaki unakuwa rahisi na vibali vitolewe kwa ngazi ya kijiji kwa wachimbaji wadogo.

Akijibu swali hilo, Dk. Kiruswa alisema mradi huo unafadhiliwa na Benki ya Dunia (WB) na kutekelezwa chini ya Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

Aidha, alisema wizara hiyo imeendelea kufanya jitihada mbalimbali ili kuimarisha usimamizi, upatikanaji na matumizi ya baruti hapa nchini.

"Ili kurahisisha upatikanaji wa vibali vya baruti, wizara imesogeza huduma hiyo katika ofisi za maofisa madini wakazi wa mikoa yote ya kimadini nchini ikiwamo Chunya. Serikali imesajili na kutoa vibali vipya vya biashara ya baruti kwa kampuni 25 ambazo hutoa huduma hiyo hapa nchini," alisema.

Alibainisha wizara hiyo katika kipindi cha mpito kwa matumizi ya zebaki imeendelea kufanya jitihada mbalimbali ikiwamo, kushirikiana na Ofisi ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, kufanya ufuatiliaji wa taratibu za uingizaji na usambazaji wa kemikali ya zebaki nchini ili kubaini changamoto za upatikanaji wa kemikali hiyo.

"Kuandaa takwimu za kiasi cha matumizi ya zebaki ili kujua kinachohitajika nchini ili kurahisisha utoaji wa vibali vya uingizaji na kuwatambua na kuwasajili waingizaji na wasambazaji wa kemikali ya zebaki nchini kwa mujibu wa Sheria ya Kemikali nchini ili biashara hiyo ifanyike kwa uwazi," alisema.

Aidha, alisema pamoja na kemikali ya zebaki kutumika katika shughuli za ukamatishaji wa dhahabu, utafiti wa kisayansi umebainisha kuwa kemikali hiyo isipotumika vizuri ni hatari kwa afya za binadamu na mazingira.

"Kutokana na hali hii serikali imesaini mkataba wa Minamata ambao utekelezaji wake unasababisha kupunguza matumizi ya zebaki au kuondoa kabisa pale inapowezekana," alisema.

# Mbunge ahoji wigo uboreshaji barabara mitaa Dar

MBUNGE wa Temeke (CCM), Dorothy Kivale, amehoji serikali ina mikakati gani ya kupanua wigo wa miradi ya kuboresha barabara za mitaa ya Manispaa ya Temeke kupitia Mradi wa uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam (DMDP).

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, alisema ofisi hiyo imewasilisha mapendekezo ya kujengwa mtandao wa barabara za Manispaa ya Temeke wenye jumla ya kilomita 53.10 ya kiwango cha lami.

Alibainisha kuwa fedha hizo zimeombwa Wizara ya Fedha na Mipango ili iwe sehemu ya mzunguko wa 20 wa mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia katika Mkoa wa Dar es Salaam, unaotarajia kuanza mwezi Julai 2022.

"Serikali kupitia mradi wa DMDP awamu ya kwanza inajenga mtandao wa barabara wenye jumla ya kilomita 48.243 kwa gharama ya Sh. bilioni 60.9 katika Jimbo la Temeke kwa Kata za Mtoni kilomita 9.623," alisema.

Aidha, alisema Makangarawe kilomita 10.402, Yombo Vituka kilomita 7.710, Kilakala kilomita 10.53, Keko kilomita 0.462, Buza kilomita 1.7 na Kata za Changombe, Sandali, Temeke na Azimio zimejengwa kilomita 7.8.

"Kwa sasa kilomita 46.543 zimekamilika na zinatumika na kilomita 1.7 za Buza zilizosalia zinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Septemba, 2022," alisema.

Alifafanua kuwa kupitia Mradi wa DMDP Awamu ya Pili katika Jimbo la Temeke, imependekezwa kujengwa mtandao wa barabara wa kilomita 53.10 kwa kiwango cha lami zinazokadiriwa kugharimu Sh. bilioni 69.5.




**Habari zote: Augusta Njoji , DODOMA**

## Katibu Mkuu Chongolo anapotoa ya moyoni

Ukurasa 13



Ukurasa 14



## HASSAN SHEIKH MOHAMUD RAIS ALIYECHAGULIWA MARA 2 KUONGOZA TAIFA KAZI KUBWA KUUNGANISHA WANAMGAMBO SOMALIA



# Mgogoro wa NCCR-Mageuzi umefikia hapa

## •Makada waliokengeuka kuwekwa kiti moto

**Na Sabato Kasika**

MVUTANO wa uongozi ndani ya chama cha NCCR-Mageuzi, umechukua sura mpya kufuatia upande wa Mwenyekiti aliyewekwa pembeni, James Mbatia, kujipanga kuwaita ili kuwahoji wahusika.

Wote waliotangaza kumwengua katika nafasi ya mwenyekiti wa taifa sasa wataitwa ili wajieleze.

Hayo ni maelezo ya Mkuu wa Idara ya Uenezi na Mahusiano ya Umma wa chama hicho, Edward Simbeye, kwa waandishi wa habari aliyoyatoa Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.

Kwa nini wamefikia hatua hiyo? Ni kutokana na kile anachosema kuwa chama kimepokea barua ya wito ya Msajili wa Vyama vya Siasa ya kutaka kukutana naye mwezi huu ili kujadiliana kwa kina mgogoro huo.

"Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa imetuandikia barua ya kutaka kukutana na mwenyekiti wetu na inamtambua kwani iemtaja kama mwenyekiti, hivyo kikao cha kumwengua hakikuwa halali,"anasema Simbeye.

Mkuu wa Idara ya Uenezi na Mahusiano ya Umma, anaongeza kuwa kwa hatua hiyo ya kumtambua, sasa watawaita wale wote walioitisha kikao Kurasini na kutangaza kumwengua Mbatia ili wajieleze kwa nini walifanya hivyo na lengo lao lilikuwa nini?

"Msajili anataja pande mbili, lakini sisi tunaamini kwamba NCCR -Mageuzi hakuna pande mbili bali kuna watu waliokengeuka, hivyo tunawashughulikia kwa mujibu wa katiba ya chama, taratibu kanuni na sheria," anaongeza

Simbeye anasema chama kina taratibu zake za ndani, na kwamba watawajibishana kwa mujibu wa katiba yao ili kuhakikisha haki ina tendeka kwa kila aliyehusika na kile alichokiita uhuni, kuhojiwa kusikilizwa naye kueleza yake.



Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi Taifa, James Mbatia aliyedaiwa kuondolewa kwenye nafasi hiyo. **PICHA: MTANDAO**

### OMBI KWA MSAJILI

Anasema, Msajili wa vyama ya siasa amewaita wakutane Juni 21 mwaka huu ili kuwekana sawa, lakini wao wanaomba kikao kisogezwe karibu ili wamalizane waendeelee na shughuli za chama.

"Msajili ametuita ili tukutane naye Juni 21, hatutakataa wito, ila huko ni mbali sana, tumemwandikia barua ya kuomba kukutane naye mapema zaidi, kwani tumesimamisha shughuli za chama kwa muda mrefu,"anasema Mkuu wa Idara ya Uenezi na Mahusiano ya Umma.

Kiongozi huyo anaongeza kuwa wanaomba msajili awaruhusu wakutane naye wiki hii badala ya kusubiri hadi Juni 21, ambayo wao wanaona ni mbali na kwamba shughuli za chama zitaendelea kusimama.

Anasema, huo ndiyo ufafanuzi wa madhila yaliyokikumba chama hicho mwezi uliopita na kwamba sasa kila kitu kinakwenda vizuri baada ya Ofisi ya Msajili kumtambua Mbatia kama Mwenyekiti wa Taifa wa chama hicho.

"Hivyo nirudie kusema kuwa tunaomba tukutane na Msajili wa Vyama vya Siasa mapema badala ya Juni 21 ambayo tunaiona kuwa ni mbali sana kwani ofisi ya chama imefungwa shughuli zimesimama," anasema.

### CHANZO CHA MGOGORO

Hivi karibuni, mjumbe wa Halmashauri Kuu na kinara wa azimio la kumwengua Mbatia, Joseph Selasini, alitangaza uamuzi huo ulioambata na kuvunjwa kwa Baraza la Wadhamini la NCCR- Mageuzi.

Katika uamuzi huo, waliteuliwa wajumbe wapya ambao watasajiliwa kwa mujibu wa taratibu zitakazowekwa, huku Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza, akikiri kupokea barua kutoka NCCR-Mageuzi kuwa kuna mabadiliko ya wajumbe wa bodi ya wadhamini.

Baada ya tamko hilo, ndipo muda mfupi baadaye Katibu Mkuu wa NCCR-Mageuzi, Martha Chiomba, alifunga ofisi za chama hicho zilizopo Ilala, Dar es Salaam, ili kumzuia James Mbatia.

Kufuatia tukio hilo, wanachama wanaomuunga mkono Mbatia, walifika ofisini hapo na kuzungumza na wanahabari wakisema waliotangaza kumsimamisha hawana mamlaka na pia akidi haikutimia.

Tukio hilo lilimwibua Simbeye ambaye alitamka kuwa kilichofanyika ni uhaini na uhuni ndani ya chama na kusema hawawezi kukubali, na kwamba chama kitakaa na kufanya maamuzi, na kusikitishwa na Msajili wa Vyama vya Siasa kushiriki katika tukio hilo.

Lawama zilielekezwa kwa Sisty Nyahoza kuwa ndiye anaendesha makundi na kuyafadhili huku akidai kuwa ukifika wakati wataweka ushahidi hadharani wa tuhuma hizo.

KUELEKEA UCHAGUZI MKUU

# Dalili zote zinaonyesha ni msimu wa 'baba Odinga,' ila....



Baada ya kumpinga, mgombea Raila Odinga, Kalonzo Musyoka anaeleza kuwa , amerudi nyumbani kuungana na Baba Raila. **PICHA MTANDAO.**

**Na Ani Jozeni**

UCHAGUZI mkuu nchini Kenya unatazamiwa kufanyika katika miezi miwili ijayo, na harakati za kampeni zinaendelea kupamba moto , wakati ambao ndiyo kwanza orodha ya wagombea inaendelea kukamilishwa na Tume ya Uchaguzi na Mipaka ya Majimbo, kuhusu nani atagombea nafasi gani.

Kilichokuwa kinangojewa zaidi ni wagombea urais, huku baadhi ya wanasiasa waandamizi waliotaka kuingia katika kinyang'anyiro kama wagombea huru walikwama.

Sababu ni kuwa walishaingia mikataba na makundi muhimu mawili yanayotoa wagombea, na muda wa makubaliano hayo kuanza kuhojiwa haujapita bado.

Suala hapa ni vikundi vya kisiasa ama hata mtu mmoja mmoja wana uwezo wa kuamua wanachotaka katika uchaguzi, lakini hata hivyo lazima visajiliwe ili viwe na nguvu kikatiba, kuwa nani yuko upande gani wakati wa kampeni na wa kupiga kura.

Walioingia katika matatizo ya aina hiyo, kati ya wale waandamizi zaidi, ni Musalia Mudavadi anayetokea upande wa magharibi wa nchi hiyo na ambaye kadhalika ni mfuasi wa Naibu Rais William Ruto, na Kalonzo Musyoka, ambaye sasa 'amerudi kundini,' akimuunga mkono Raila Odinga.

Ni baada ya kukwama katika mkakati wa kugombea kama mtu huru na binafsi, hivyo akaona ajiunge na 'wanaouzika,' au kukubalika kambi ya 'baba,' Raila.

'Baba' ndiye mgombea muhimu katika uchaguzi wa mwaka huu kwani ana hadhi tofauti ya kisiasa, kuwa siyo tu mgombea ila alikuwa kiongozi wa upinzani mwenye daraja la mshauri mkuu wa Rais Uhuru Kenyatta wakati wa muhula wa pili.

Ilibidi kufikia hapo kwa sababu kulikuwa na dalili za kuvunjika kwa amani endapo maridhiano yasingefikiwa, kwani Raila Odinga aliapishwa kama 'rais mbadala wa watu wa Kenya' na mwanasheria-mwana harakati Miguna Miguna ambaye serikali ilimfukuza nchini humo akitakiwa arudi Canada kwani ana uraia pacha.

Kupeana mikono, maridhiano, kulibadili sura ya siasa nchini, inayoasisiwa na kuendelezwa na Raila na Rais Uhuru Kenyatta.

Wakati Raila akiwa mshauri mkuu wa Rais Kenyatta, aliteuliwa msimamizi mkuu wa shughuli za serikali ambaye pia ni Waziri wa Mambo ya Ndani, ambaye kimsingi alikuwa kama Waziri Mkuu.

Ni muundo wa kuendesha serikali usiokuwa wa kawaida lakini uliwezesha mambo kwenda vyema na maandalizi kufanyika ya kumritisha kiti hicho Odinga.

Licha ya umri wake mkubwa haikuwezekana kupatikana mtu ambaye Rais angeridhika naye, au kuwa na hoja za kutosha kwa wapiga kura wake wa mwaka 2018, kwanini awe huyo na siyo Naibu wake, William Ruto.

Ingebidi awe mtu ambaye ni kama yuko chama kimoja na Kenyatta, ila chama hicho siyo cha kisiasa bali mtandao wa maelewano kati ya mkuu wa nchi na upinzani.

Kuteuliwa kwa Martha Karua, mwandani au mshauri wa karibu wa hayati Mwai Kibaki, aliyeongoza nchi hiyo awamu ya tatu, ni hatua ambayo imemsaidia 'baba' kwani ukanda wa kati wenye wapiga kura wengi wa Kikuyu umeridhika na uteuzi wake.

Kulikuwa na mvutano kati ya uteuzi huo na Musyoka, ambaye wakati wa awamu hiyo ya tatu alikuwa Makamu wa Rais akishindana kwa kumshauri rais na hata kufanya maamuzi, na Odinga, aliyekuwa Waziri Mkuu katika serikali nyingine ya maridhiano.

Popote yalipo maridhiano, Odinga yupo, na mwisho wa awamu ya pili alikuwa Katibu Mkuu wa KANU kilichokuwa chama tawala ila 'maridhiano' hayakufikisha Rais Daniel Arap Moi, kumteua kugombea, akampendekeza Uhuru Kenyatta.

Profesa huyo wa siasa alijua wazi 2006, lakini angeweza kubuni kuwa labda baadaye angeweza kufikia kiti hicho. Na ni kweli aliingia kitini alipoondoka Kibaki, na sasa aliyekataliwa na Moi anakuwa ndiye mbadala wa kukubalika kama Uhuru alivyokuwa wakati ule, ila kwa 'kazi ya mikono' ya 'kujenga madaraja' kati ya makundi hasimu ya nchi hiyo.

Lengo muhimu lilikuwa ni kumaliza siasa za kikabila zinazoisumbua Kenya tangu uhuru, ila lazima kuwepo angalizo, kuwa kabila ni suala moja na jingine ni sera, nani anaweza kulinda mfumo uliopo.

Ndipo wataona tofauti kati ya chaguzi zilizopita na uchaguzi huu, kuwa siasa za kikabila zimepungua nguvu na zile za sera zimeongezeka, kwa mfano viongozi waandamizi wa ukanda wa kati wakiunga mkono msimamo wa Rais Kenyatta kumuunga mkono Raila walisema hawapo tayari kuona 'mafisadi wanakamata nchi,' kwani kundi hilo jingine limeandamwa na shutuma kuwa hawakerwi na uporaji au udanganyifu katika matumizi ya fedha za serikali.

Wanachofanya wao ni kucheka tu, kuwa matamshi hayo yana ajenda ya kisiasa, kumchafulia jina mgombea anayetafuta kurithi kiti hicho, yaani Ruto.

Kinachoshangaza kiasi fulani katika uchaguzi huu ni kuwa ambaye yuko madarakani kati ya wagombea wawili amekuwa ndiyo mpinzani, na aliyeko upinzani ila kwa ushirikiano mzuri sana na anayeondoka madarakani, ndiye anawakilisha serikali iliyoko madarakani.

Kwa maana hiyo 'mpinzani Ruto'anakuwa na uwezo wa kuahidi 'mabadiliko' kuliko Raila kwani 'baba'ni mgombea anayesimama pale alipo Rais Kenyatta, wakati Naibu Rais Ruto anatumia kila nafasi kueleza asivyotendewa haki.

Ila hivi karibuni alifanya tendo la uungwana wa kisiasa lililowashangaza wengi, katika hafla ya ibada ya kitaifa ambako alikuwa anaongea kwa mara ya mwisho kanisani kama Naibu Rais, na Uhuru kwa mara ya mwisho kama Rais.

Kwanza alimkaribisha bila kutarajiwa Martha Karua kuongea na hadhara hiyo, akiwa tayari ni mgombea mwenza wa Odinga, akabuni haraka haraka cha kusema, na akawaridhisha wasikilizaji wake.

Ruto pia alichukua nafasi hiyo kumwomba radhi Uhuru pale ambapo hakufikia matazamio yake akifanya naye kazi kama naibu wake , hatua iliyoshangaza wengi na kuthibitisha kuwa licha ya yote, ni muungwana.

Uhuru hakuwa na la kusema moja kwa moja kwa ridhaa hiyo, akamtakia mema 'mheshimiwa Ruto' na kuahidi kuwa watakutana hivyo hivyo mbele ya safari, akiwa na maana mapambano yanaendelea.

# Katibu Mkuu Chongolo anapotoa ya moyoni

## •CCM tuna jambo letu miradi ya kimkakati

**Na Maulid Mmbaga**

ILI kukabiliana na uzembe unaokwamisha miradi ya maendeleo ikiwamo ya kimkakati, viongozi wa CCM wamekuja na utaratibu wa kutembelea na kukagua kila mradi ili kufuatilia ufanisi na ukamilishaji wake.

Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, ameyasema hayo katika ziara ya hivi karibuni kwenye mikoa ya Shinyanga na Simiyu na kuhimiza kuharakishwa utekelezaji wa miradi ya kimkakati ukiwamo wa kusambaza maji kutoka Ziwa Victoria kwenda mikoa ya kanda ya ziwa.

Ndani ya ilani ya CCM moja ya vipaumbele ni pamoja na kuanzisha, kutekeleza na kukamilisha miradi ya kimkakati inayolenga kuinua uchumi na kumgusa kwa kumnufaisha kila Mtanzania.

Hata hivyo, lengo hilo linaweza kukwamishwa na baadhi ya watendaji wenye dhamana ya kusimamia miradi hiyo, lakini wanashindwa kutekeleza majukumu yao kikamilifu na kuzorotesha maendeleo ya taifa. Ndiyo maana imekuja na mkakati wa kufuatilia kila hatua.

Baadhi ya miradi kutokukamilika kwa wakati na mingine kujengwa chini ya viwango ni hujuma, hasara kwa taifa lakini pia husababisha wananchi kukosa huduma wanazostahili na kwa wakati, anasema Chongolo.

Miongoni mwa miradi ambayo Katibu Mkuu anaipa nguvu mpya anapotembelea Simuyu na Shinyanga ni ukamilishaji wa hospitali za maeneo mbalimbali wilayani Ushetu mkoani Shinyanga, kujenga barabara pamoja na mradi wa reli ya kisasa ya mwendokasi (SGR).

Katika ziara ya hospitali ya Ushetu, Chongolo anakutana na changamoto ya ukosefu wa dawa na vifaa tiba hali ya kuwa majengo yalishakamilika na kutoa maelekezo kwa Bohari ya Dawa (MSD) kutatua tatizo hilo haraka iwezekanavyo.

Maelekezo yake hayakuishia hapo, anayafikisha pia kwenye kuharakisha ujenzi wa shule, barabara pamoja na SGR, miradi ya kusambaza maji ya Victoria na kusimamia kiwanda cha kutengeneza chaki akitaka kazi hizo zikakamilike kwa wakati na kwa thamani halisi ya fedha zilizotolewa na serikali.

Pia Katibu Chongolo, akiwa Busega mkoani wa Simiyu anaahidi kusaidia utatuzi wa changamoto ya uhaba wa watumishi wilayani humo ,lakini akiwataka waliopewa mamlaka kuacha ubaguzi na upendeleo wakati wa kuwapangia watumishi wapya vituo vya kazi, badala yake watekeleze jukumu hilo kwa mujibu wa sheria, kanuni ,miongozo na uadilifu.

"Tuache kuwapeleka watu kwa upendeleo kwenye vituo vya kazi, wakija waende wakajifunze na wakafanye kazi ambayo wananchi wanataka kupewa huduma kutoka kwao, tusiwarundike kwenye hospitali ya wilaya na vituo vilivyopo mijini tuwapeleke sehemu zote kwa sababu kote ni Tanzania na wamekubali kwenda kuwatumikia Watanzania popote walipo," anasema Chongolo.



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Daniel Chongolo akishiriki ujenzi wa Shule ya Sekondari Mwandu Itinje wilayani Meatu mkoa wa Simiyu. **PICHA: MAULID MBAGA**

Vile vile anamgeukia mbunge wa Itilima, Njalu Silanga, akimtaka kuwawezesha wakulima wa eneo hilo na kuhakikisha kila tarafa inapata mashine ya kukamua alizeti ili kuliongezea thamani zao hilo ambalo kwa mkoa huo Itilima inaongoza kwa uzalishaji wake.

### UFUMBUZI TEMBO

Akiwa wilayani Meatu huko Simiyu, Chongolo anatoa mwezi kwa viongozi wanaosimamia wanyamapori kutatua tatizo la tembo wanaoingia mashambani na kusababisha uharibifu wa mazao na kutishia maisha na maendeleo.

Kero hiyo imekuwa ikiwasumbua wananchi wa eneo hilo kwa miaka mitatu sasa, ambapo siku mbili baada ya kiongozi huyo kutoa maelekezo hayo, anaeleza kuwa hazina imeshatoa fedha na wizara husika imeshaanza kutekeleza mikakati ya kumaliza tatizo hilo, ikiwamo kujenga vibanda vya askari wa wanyama pori kudhibiti wanyama hao.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Meatu Dakawa, Msoleni, anasema wamechukua hatua mbalimbali ikiwamo kutoa elimu kwa wananchi walioko maeneo yanayopakana na yanayovamiwa na tembo.

"Kwa wale ambao wako karibu na pori la akiba la Maswa tumetoa elimu na vifaa vya kujihami kama matarumbeta, tumegawa tochi kwa ajili ya kufukuzia tembo .

Kaimu Ofisa wa Wanyamapori Wilaya ya Meatu, Deusdedith Martin, anasema hatua za haraka wanazozichukua ni kuongeza askari wa wanyamapori kutoka vituo vingine ili kuimarisha udhibiti, huku akiahidi kuwa wataendelea kudhibiti na kutoa elimu.

> "Wanyama hawa wamekuwa wakitusumbua kwa muda mrefu, mazao yetu yanaharibiwa, nguvu zetu zinapotea bure, hivyo tunamshukuru Katibu Mkuu kufika Meatu kusaidia tatizo hili kupatiwa ufumbuzi," anasema Chami.

### KAULI YA WANANCHI

Mussa Chami mkazi wa Meatu mmoja wa waathirika wa uvamizi wa tembo anamshukuru Chongolo kwa kuwapazia sauti ambayo imeonyesha matokeo ndani ya muda mfupi.

"Wanyama hawa wamekuwa wakitusumbua kwa muda mrefu, mazao yetu yanaharibiwa, nguvu zetu zinapotea bure, hivyo tunamshukuru Katibu Mkuu kufika Meatu kusaidia tatizo hili kupatiwa ufumbuzi," anasema Chami.

Emmanuel Gutta mkazi wa Ushetu mkoani Shinyanga anasema katika eneo hilo walikuwa wakikabiliwa na changamoto ya ukosefu wa dawa na vifaa tiba katika hospitali ya wilaya jambo lililokuwa likisababisha kutembea umbali mrefu kufuata huduma ya matibabu.

Anaongeza kuwa kitendo cha kiongozi huyo kufika katika eneo hilo kimesaidia kutokana na maelekezo yaliyotolewa ambayo wanatarajia yatatatua changamoto zinazowakabili.

### WITO NA MAELEKEZO

Chongolo akiwa wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, amewataka viongozi na wasimamizi wa miradi ya maendeleo kutumia kwa uadilifu fedha zinazotolewa ili kutekeleza miradi ya kipaumbele inayowagusa wananchi na kuikamilisha kwa asilimia 100.

Pia amewataka wachimbaji wadogo wa madini kuzingatia utunzaji wa mazingira na miundombinu kwa kujiepusha kuchimba sehemu inapopita miundombinu ya maji.

"Sio kila eneo linatakiwa kuchimbwa au kutumiwa kwa kila kitu, lazima mhifadhi maeneo machache kwa ajili ya matumizi maalumu ya uhifadhi, kwa wale wachimbaji wa madini, sehemu unapopita mtandao wa maji na mabomba msiende kuchimba na kuyakatakata, lindeni miundombinu hiyo," anasisitiza Chongolo.

Aidha, anaitaka Kampuni ya Uhandisi ya China (CCECC) ambayo inatekeleza mradi wa SGR kukamilisha kazi kwa wakati akitahadharisha kuwa kuchelewa kwake kunaisababishia hasara serikali.

### WANAOWABAGUA WATOTO

Akiwa mkoani Simiyu Chongolo pia amekemea tabia ya baadhi ya wazazi wanaowabagua watoto wa kike na kuwalazimisha kuolewa lengo likiwa ni kupata ng'ombe wa mahari.

Anasema serikali imejenga madarasa na shule nyingi kwenye maeneo mbalimbali, huku akibainisha kuwa kwenye jimbo la Maswa Magharibi, kumekuwa na changamoto ya kuwabagua watoto wa kike kwa kutowapeleka shule na kuwalazimisha kuolewa utotoni.

"Watoto wa kike sio mtaji wa kupatia ng'ombe, wanastahili kusoma kama ilivyo kwa wanaume, wasiposoma mnawageuza kuwa daraja la kuumizwa na kutumikishwa bila kuwa na uwezo wa kutafakari na kujiamulia wenyewe," anasema Chongolo.

### MCHAMBUZI APONGEZA

Mchambuzi wa masuala ya siasa na uchumi na mhadhiri wa Chuo cha Diplomasia, Abbas Mwalimu, anasema utaratibu wa viongozi kwenda kukagua miradi ya maendeleo pamoja na kuongea na wananchi ni sehemu ya majukumu.

Anasema utaratibu huo pia unasaidia kujiridhisha na taarifa anazopatiwa juu ya mwenendo wa utekelezaji wa miradi husika, akibainisha kuwa kumekuwa na changamoto ya utekelezaji wa miradi kwa kiwango kisichokidhi vigezo na kusababisha baadhi ya miradi iliyoanzishwa kuharibika.

"Baadhi ya watendaji siyo waaminifu, hawatoi taarifa sahihi, na kuna tatizo la kukosa uadilifu, hivyo kwa kiongozi kwenda kukagua miradi inampa nafasi ya kujiridhisha zaidi na inawapa chachu wasimamizi kujenga miradi na kuhakikisha inakidhi vigezo," anasema na kuongeza:

"Tija ipo kwa viongozi kutembelea maeneo mbalimbali, inaleta uwajibikaji na ukamilishaji wa miradi ya maendeleo, pia kuna haja ya miradi kukaguliwa tangu inapoanza, kuhakikisha kuwa vifaa vinavyotumika vinakidhi vigezo, kila hatua ikaguliwe isingojwe ukamilike, hiyo itasaidia makosa". Ameshauri Mwalimu.

Anaongeza kuwa utaratibu huo wa viongozi kwenda kukagua miradi ya maendeleo na kushuka kuongea na wananchi na kawaida ni mzuri na unasaidia kujua changamoto zinazowakabili na kuzitafutia suluhu.

## HASSAN SHEIKH MOHAMUD

# RAIS ALIYECHAGULIWA MARA 2 KUONGOZA TAIFA KAZI KUBWA KUUNGANISHA WANAMGAMBO SOMALIA



**NA MWANDISHI WETU**

UNACHOWEZA kusema ni Hassan Sheikh Mohamud ni king'ang'anizi, ni baada ya kurejea tena ikulu mjini Mogadishu kuwa Rais wa Somalia, katika awamu nyingine.

Awali alikuwa rais wa zamani wa Somalia aliyeshindwa katika uchaguzi wa 2017 na kukaa pembeni lakini akitamani kurudi sasa amechukua usukani, baada ya miaka mitano.

Amerejea madarakani baada ya kumshinda rais Sheikh Sharif Ahmed au Farmaajo (inasomwa Farimajoo), katika kinyang'anyiro cha muda mrefu kilichoamuliwa na wabunge katika duru ya tatu ya kupiga kura mwezi uliopita.

Kiongozi huyo wa zamani wa upinzani alichukuliwa kuwa mgombea jamii ya "farasi mweusi dark horse", ambaye hafahamiki sana nyenzo zake lakini anayeweza kupindua meza. Iliripoti Al-Jazeera

Mohamud alishika nafasi ya pili kwa rais aliyekuwapo madarakani, Sheikh Sharif Ahmed au' Farimajoo ', katika duru ya kwanza ya kupiga kura miongoni mwa wabunge wa Somalia.

Lakini akavuka kiwango cha asilimia 50 katika duru ya pili, na kushinda kwa kishindo kwa kura 190 dhidi ya 79 za Farimajoo.

"Moja ya matatizo tuliyo nayo hapa Mogadishu ni kuongezeka kwa vikundi vya wanamgambo wenye silaha, na nchi inahitaji mtu ambaye anaweza kuwaunganisha, kwani kuna wa Bernard Membe. kunaweza kuwa na mapigano kati ya wanamgambo hao wenye silaha.

Ilitarajiwa kwamba kura ya urais, ya kwanza ya aina yake katika miongo kadhaa, ingebadilisha hali ya kisiasa ya taifa hilo na kuwa hatua muhimu katika azma ya nchi hiyo iliyoharibiwa na vita na kukomesha miongo miwili ya ghasia, ufisadi na mapigano ya wanamgambo wanaohasimiana.

> "Moja ya matatizo tuliyo nayo hapa Mogadishu ni kuongezeka kwa vikundi vya wanamgambo wenye silaha, na nchi inahitaji mtu ambaye anaweza kuwaunganisha, kwani kuna wasiwasi kwamba kunaweza kuwa na mapigano kati ya wanamgambo hao wenye silaha.

**HISTORIA YA MOHAMUD**

Alizaliwa mwaka 1955 katika mji wa Jalalaqsi karibu na Mto Shebelle katikati ya Somalia. Ni msomi, aliyehitimu nchini Marekani na India.

Amekuwa mhadhiri wa chuo kikuu, akifanya kazi Benki ya Dunia (WB) na Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP) na pia akitumika na asasi za kiraia za Somalia tangu 2008.

Ni mtunzi mwaka 2009 alichapisha kitabu kuhusu historia ya upatanishi nchini Somalia .

Alianzisha chama cha siasa cha Amani na Maendeleo mwaka 2011 akiwa mwasisi na mwenyekiti wa kwanza.

**MADARAKA YA URAIS**

Aliiongoza Somalia kati ya mwaka 2012 na 2017, mwezi uliopita alishinda uchaguzi huo katika mji mkuu Mogadishu, wakati kukiwa ulinzi mkali uliowekwa na mamlaka ili kuzuia mashambulizi makali ya wanamgambo wa itikadi kali.

"Linapokuja suala la chuki za aina yoyote, niko tayari kuzitatua, kama tu nilivyosema wakati natangaza kugombea urais mwanzoni mwa wiki hii. Hakuna kisasi wala ufuatiliaji wa kisiasa unaomlenga mtu yeyote. Nchi hii ina kanuni na sheria za kutosha na kama tofauti zozote zikitokea, tutapitia sheria zilizotungwa na nchi hii." anasema Mohamud, mapema mwezi uliopita.

Akisema yaliyotokea ni ushindi wa watu wa Somalia. Anaongeza kuwa ushindi huo ni watu wa Somalia, na huo ni mwanzo wa enzi ya umoja, demokrasia ya Somalia na mwanuzo wa vita dhidi ya rushwa.

Alitamba kuwa anaona kazi ngumu mbele baada ya kushinda urais huo.

Katika duru ya kwanza ya kupiga kura ilikuwa na wagombea 36, ambapo wane walisonga hadi duru ya pili. Baada ya kukosekana mshindi aliyepata angalau theluthi mbili ya kura 328, upigaji kura kisha ukaingia katika duru ya tatu ambapo ushindi wa zaidi ya nusu ya kura ulitosha kumchagua mshindi

Wajumbe wa mabaraza mawili ya bunge walimchagua rais katika kura ya siri iliyopigwa ndani katika uwanja wa ndege wa kambi ya jeshi ya Halane, ambayo inalindwa na walinda amani wa Umoja wa Afrika.

Kuchaguliwa kwa Mohamud kumekamilisha mchakato wa uchaguzi uliocheleweshwa kwa muda mrefu ambao uliibua mivutano ya kisiasa na ongezeko la wasiwasi wa ukosefu wa usalama, baada ya muhula wa Rais Mohamed Abdullahi Mohamed kumalizika Februari 2021 bila kuwepo na mrithi wake.

**FARMAAJO AKIRI KUSHINDWA**

Rais aliyeondolewa Mohamed, maarufu kama Farmaajo alikiri kushindwa, na Mohamud akaapishwa mara moja.

Mohamud (66), ni kiongozi wa chama cha Union for Peace and Development ambacho kina wingi wa viti katika mabaraza yote mawili ya bunge.

Anatokea ukoo wa Hawiye, mojawapo ya koo kubwa zaidi Somalia, na anaelezwa kuwa ni kiongozi wa taifa mwenye mtizamo wa upatanisho.

Wasomali wengi wanatumai Mohamud anaweza kuiunganisha nchi baada ya miaka mingi ya mivutano ya koo zilizogawika lakini pia kuchukua usukani thabiti wa serikali ya shirikisho ambayo inakabiliwa na kukosa uwezo wa kudhibiti majimbo mengine zaidi ya Mogadishu.

Wachambuzi walikuwa wamebashiri kuwa Mohamed angekabiliwa na vita vikali ili kuchaguliwa tena. Hakuna rais aliyeko madarakani ambaye amewahi kuchaguliwa kwa mihula miwili mfululizo katika taifa hilo la upembe wa Afrika, ambako koo pinzani hupigania vikali madaraka ya kisiasa. Katika kushinda uchaguzi huo hata hivyo, Mohamud ameweka historia kwa sababu hakuna rais wa zamani aliyewahi kufanikiwa kurejea madarakani.

Lengo la kufanya uchaguzi wa moja kwa moja, wa mtu mmoja kura moja nchini Somalia, nchi yenye watu milioni 16, bado gumu kwa kiasi kikubwa kutokana na mashambulizi makali ya itikadi kali. Maofisa walikuwa wamepanda kuwa na uchaguzi wa moja kwa moja mara hii lakini, badala yake, serikali ya shirikisho na majimbo wakakubali kuwa na "uchaguzi mwingine usio wa moja kwa moja," kupitia wabunge waliochaguliwa na viongozi wa jamii - wajumbe wa koo zenye nguvu - katika kila jimbo mwanachama.

***DW/ ALJAZEERA***



## Serikali kuendelea kutafutia mikopo wanafunzi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema inaendelea na jitihada za kutafuta mikopo kwa ajili ya kuwakopesha wanafunzi wa vyuo vya kati na ufundi nchini.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alibainisha hayo juzi alipokuwa akifunga maonyesho ya elimu ya sayansi na mafunzo ya ufundi stadi TVET, yaliyofanyika jijini Dodoma.

Alisema, jitihada ambazo serikali inaendelea kufanya ni kutafuta mikopo na benki ya NMB imekubali kutoa Sh. bilioni 200 kwa ajili ya kukopesha wanafunzi wanaosoma vyuo vya kati na ufundi nchini.

"Mikopo hii haitakuwa kama ile inayotolewa na Bodi ya Mikopo kwa hiyo kama ni mfanyakazi atahitaji kumsomesha mtoto wake VETA atapewa mkopo huo kwa masharti nafuu," alisema Prof. Mkenda.

Alisema katika kuhakikisha zoezi la kutoa mikopo katika ngazi hiyo linakuwa kwa ufasaha inahitajika kuwa na takwimu mahususi za vyuo vyote vinavyotoa mafunzo.

"Tukiwa na takwimu sahihi tukajua ni kozi gani ambazo wanafunzi wakisoma wanaajiriwa haraka tunaweza kuongea na benki zetu wakatoa mikopo kwa wanafunzi hao na watarejesha wenyewe watakapo ajiriwa au kujiajiri hii itasaidia kupanua wigo wa wanafunzi wanaomaliza vyuo na kujiajiri au kuajiriwa," alisema.

Aliwaagiza Baraza la Elimu ya Sayansi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET), kuhakikisha wanasimamia maudhui yanayotolewa katika vyuo ili kuendelea kutekeleza maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa wakati akihutubia Bunge.

"Rais Samia wakati akihutubia bunge aliagiza Wizara ya Elimu kupitia sera na mitaala ya elimu ili kuongeza ubora wa elimu kuhakikisha inayotolewa inaleta ujuzi ili kumwandaa mhitimu kumudu mazingira na aweze kuajirika na kujiajiri," alisema.

Katibu Mtendaji wa NACTVET, Dk. Adolf Rutayuga, alisema katika kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa elimu ya mafunzo stadi yenye ubora hadi kufikia Juni 2022, baraza lilikuwa limesajili vyuo 454 vya elimu ya ufundi.

Alisema kati ya vyuo hivyo 179 ni vya serikali na 275 ni vya sekta binafsi.

"Idadi ya wanafunzi wanaojiunga na vyuo hivyo imeongezeka kutoka 117,474 katika mwaka wa masomo 2014/2015 hadi kufikia 210,775 mwaka 2020/2021 ikiwa ni ongezeko la wanafunzi wengi zaidi hasa katika vyuo vya sekta binafsi ambavyo vimekuwa na mchango mkubwa," alisema.

# Utekelezaji programu kukuza ujuzi wa kujiajiri waanza

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeanza kutekeleza programu ya kukuza ujuzi wa kujiajiri (ESP), inayogharimu Sh. bilioni 45.4 inayolenga masuala mbalimbali ikiwamo kuimarisha maeneo ya elimu kwa wasichana waliokatisha masomo. Programu hiyo itafanyika kwa miaka saba nchini (2021-2028) na inatekelezwa na Umoja wa Taasisi na Vyuo Canada (Canada-CICan), kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Idara ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (DTVET).

Akifungua jana Warsha ya Wadau wa ESP, wakiwamo Wakuu wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs), Mjumbe wa Kamati ya Uratibu wa Programu hiyo kutoka wizara hiyo, Margaret Mussai, alisema lengo la serikali ni kupiga hatua katika masuala ya kuwawezesha wanawake ili kufikia usawa wa kijinsia na haki za binadamu.

"Vyuo FDCs ni msingi katika kukuza ujuzi kwa vijana hasa wale wenye uhitaji, lakini pia vinatumika kama njia mbadala kwa wale waliokatisha masomo kwa sababu mbalimbali na wangependa kuendelea na masomo ama kupata ujuzi wa aina fulani," alisema.

Alifafanua kuwa kiasi hicho cha fedha kitatumika kuandaa mafunzo ya ujuzi ya muda mfupi, walengwa wakuu wakiwa ni wasichana na wanawake 720, kutoa mafunzo ya jinsia na haki za binadamu kwa walimu na watumishi 180 kati yao wanawake 60 na wanafunzi 3,200 ikiwamo wasichana 1,000. "Kujenga uwezo wa kutoa huduma kama vile ushauri nasaha kwa wanawake na wasichana hasa waliozaa katika umri mdogo na kuzishirikisha jamii katika shughuli za uhamasishaji na uelimishaji kutambua faida za msichana kujiendeleza kimasomo na kumpa nafasi mwanamke kushiriki mafunzo ya kujenga na kukuza ujuzi ili kujikomboa kiuchumi wanajamii 2,400 ikiwamo wanawake 1,200 na wananchi wa kujitolea 36 watanufaika na mafunzo," alisema.

Aliahidi kuwa wizara hiyo itasimamia kikamilifu utekelezaji na kuhakikisha malengo ya programu ya kukuza ujuzi yanafikiwa na vijana wa Tanzania.

Naye Meneja Programu wa ESP kutoka CIcan-Canada, Tom Tunney, alisema anaamini ushirikiano unaoletwa na ESP utakuwa na matokeo chanya katika masuala ya usawa.

"Kuwasilisha matokeo ya uchambuzi wetu wa Usawa wa Kijinsia (GE Analysis), kuwasilisha na kupata maoni juu ya Mkakati wa Usawa wa Kijinsia (GE Strategy) ambao ni matokeo ya Uchambuzi wa Usawa wa Kijinsia (GE Analysis) na kutengeneza kwa pamoja mipango ya utekelezaji kwa hatua zinazofuata baada ya warsha hii," alisema.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, akizungumza na walengwa wa TASAF na wananchi wa Kijiji cha Bukulu wilayani Kondoa juzi, wakati wa ziara yake ya kikazi ya kukagua utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini. **PICHA: UTUMISHI**

# Vijana waitwa kuchangamkia fursa mafunzo sheria

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TAASISI ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania (The Law School of Tanzania), imetoa wito kwa vijana kuchangamkia fursa ya mafunzo ya wasaidizi wa sheria ili kuwa wabobezi kwenye masuala ya sheria. Akizungumza jijini hapo maonyesho yalioandaliwa na Baraza la Taifa na Elimu ya Ufundi na Ufundi Stadi (NACTVET), Mhadhiri Msaidizi kutoka Taasisi hiyo, Paul Rambau, alisema dirisha la kusajili kwa ajili ya mafunzo ya wasaidizi wa sheria ngazi ya cheti, limefunguliwa na mafunzo hayo yanatarajia kuanza mwezi Septemba, mwaka huu, na ni ya kwanza kutolewa na taasisi baada ya kupewa ithibati kutoka NACTVET.

Alisema mafunzo hayo yanatolewa kwa mtu yeyote ambaye amehitimu elimu ya kidato cha nne na kuendelea na mwenye ufaulu wa alama D kwenye masomo manne ya kidato cha nne ikiwamo somo la Kiingereza.

"Haya mafunzo ya wasaidizi wa kisheria ngazi ya cheti, yatatolewa na taasisi kwa muda wa mwaka mmoja miezi mitano wanafunzi watajifunza wakiwa darasani na miezi mingine mitano watajifunza wakiwa sehemu za kazi kwenye taasisi zinazotaka msaada wa kisheria, lakini miezi miwili itatumika kwa ajili ya likizo na mitihani," alisema.

Alisema kutokana na Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania kuwa ya kwanza kutoa mafunzo ya ngazi ya cheti anawasihi vijana kuchangamkia fursa hiyo.

"Niwasihi vijana wenye sifa hizi kuchangamkia fursa ya kusoma mafunzo ya wasaidizi wa kisheria mafunzo ambayo yatatolewa na wabobezi katika masuala ya sheria," alisema.

Hata hivyo, Rambau alisema, taasisi pia ipo kwenye mchakato wa kuandaa mtaala wa stashahada ambapo mwanafunzi atakapomaliza mafunzo ngazi ya cheti ataendelea mbele katika ngazi ya stashahada.

"Mafunzo yatakayotolewa yatakuwa na ubora ambao utamwezesha mwanafunzi kufanya kazi kama msaidizi wa kisheria au kuendelea mbele kimasomo kwa ngazi ya diploma ama shahada iwapo atapenda kufanya hivyo kwa kuwa cheti kitakachotolewa kitakuwa kinatambuliwa na NACTVET," alisema.



# Serikali yaagiza msako kubaini waliomuua padri

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imeliagiza Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi na kuwabaini watu wote waliohusika na mauaji ya Padri wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Mbeya, Michael Samson (63), raia wa Malawi na kuwachukulia hatua kali za kisheria.

Mwili wa Padri Michael ambaye alikuwa wa Shirika la Wamisionari wa Afrika (White Fathers), ulikutwa umetupwa chini ya daraja la Mto Meta lililoko Sabasaba jijini Mbeya ukiwa umeviringishwa kwenye blanketi na baadhi ya viungo vikiwa vimetenganishwa.

Awali padri huyo alitoweka Juni 10 mwaka huu, majira ya saa 12 jioni katika Kituo cha Vijana cha Kanisa Katoliki cha Mbeya (Youth Centre) na inadaiwa aliwaaga wenzake kwamba alikuwa anakwenda kufanya mazoezi ya kutembea.

Tangu wakati huo mtumishi huyo wa kiroho hakurejea mpaka mwili wake ulipokutwa umetupwa kwenye eneo hilo la Sabasaba na watu wasiojulikana.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema tukio hilo limezua hofu miongoni mwa wananchi wa mkoa huo, hasa viongozi wa dini, kutokana na chanzo cha tukio kutojulikana.

Alisema Jeshi la Polisi linatakiwa litumie njia mbalimbali kwenye uchunguzi ili wahusika wapatikane na hatua zichukuliwe dhidi yao huku akiwataka wananchi kutoa ushirikiano watakapotakiwa kufanya hivyo na jeshi hilo.

"Sisi kama serikali tunalaani vikali tukio hili, mkoa wetu ulikuwa umetulia sana lakini ghafla linatokea hili na bahati mbaya sana limetokea kwa mtumishi wa Mungu. Tunaliagiza Jeshi la Polisi kutumia mbinu za kiintelijensia kuchunguza tukio hili haraka sana," aliagiza.

Homera alisema wananchi wanatakiwa waendelee kuiamini serikali na Jeshi la Polisi, akisisitiza kuwa wahusika wa tukio hilo lazima watabainika na hatua za kuchukuliwa kwa kuwa baadhi ya matukio mabaya yamewahi kufanywa kwa siri lakini wahusika walikamatwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Ulrich Matei, alisema jeshi hilo linaendelea na upelelezi wa tukio hilo na uchunguzi ukikamilika, taarifa itatolewa kwa umma.

Alisema mpaka sasa wameshaanza kupata baadhi ya taarifa muhimu ambazo zinaleta matumaini ya kupata ukweli tukio hilo huku akisisitiza kuwa watazitumia taarifa zote watakazokuwa wanazipata kutoka kwenye vyanzo mbalimbali.

"Sitaki kusema vitu ambavyo tumeanza kubaini kwa sababu jambo hili bado tunalichunguza, lakini niwahakikishie mpaka sasa tumeshaanza kupata baadhi ya taarifa na tutahakikisha tunafuatilia jambo hili mpaka mwisho," alisema.

Kamanda Matei alisema wahusika wa tukio hilo wakikamatwa, watatangazwa hadharani ili iwe fundisho kwa watu wengine ambao wana tabia ya kufanya uhalifu wa aina hiyo.

Aliwataka wananchi wa Jiji la Mbeya kutoogopa kupita katika eneo hilo kwa maelezo kuwa usalama upo wa kutosha licha ya tukio hilo kuchafua sura ya eneo husika.

Juzi wananchi wa Kata ya Sisimba walikubaliana kuacha kupita katika eneo hilo hasa nyakati za usiku kutokana na mauaji ya padri huyo.

## Wananchi wataka hatua biashara za barabarani

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

WAKAZI wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya wameiomba serikali kukamilisha miundombinu ya masoko yaliyoko kwenye mji huo ili kurahisisha utendaji wa wajasiriamali wanaofanya shughuli zao kwenye hifadhi ya barabara.

Wananchi hao walisema kwenye maeneo ya barabara wanamofanyia biashara zao, ni hatari kwa maisha yao kwa maelezo kuwa wanaweza wakaparamiwa na magari yanayopita kwenye maeneo hayo.

Justo Fumbo, mmoja wa wananchi hao, alisema jioni wajasiriamali huwa wanapanga bidhaa zao kwenye barabara na kusababisha magari kushindwa kupita na hivyo kusababisha msongamano.

Alisema matumaini yake Soko la Makaburini lililoko katika Kata ya Nsalala na lile la Tambuka Reli yakikamilika, wajasiriamali hao watahamishiwa huko ili kuondoa tatizo hilo.

"Tuna historia ya matukio ya aina hii kuwahi kutokea kwenye baadhi ya maeneo katika mkoa wetu, iliwahi kutokea ajali katika Mji wa Kiwira wilayani Rungwe ambayo iliua na kujeruhi watu," alisema Fumbo.

Salome Ngoka, mmoja wa wajasiriamali, alisema wanafanyia biashara hizo kwenye eneo la barabara kwa sababu hakuna maeneo rasmi ya kufanyia shughuli zao nyakati za jioni baada ya Soko la Tarafani kufungwa.

Alisema soko hilo huwa linafungwa saa 12:30 jioni muda ambao wananchi wanakuwa bado wanahitaji huduma mbalimbali na hivyo kuamua kufanyia shughuli hizo barabarani.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, akizungumza na waandishi wa habari, mkoani humo jana, wakati wa uzinduzi wa mfumo wa kielektroniki wa utoaji wa vibali vya msimu kwa raia wa kigeni kutoka kwenye mataifa yanayozunguka Tanzania. Kushoto ni Mkuu wa Idara ya Uhamiaji wa mkoa huo, Kigongo Shile. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Uhamiaji yapata mfumo wa vibali vya msimu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

IDARA ya Uhamiaji imeanzisha mfumo wa kielektroniki wa utoaji wa vibali vya msimu (Seasonal Migrant Pass) kwa raia wa nchi nane zinazoizunguka Tanzania wanaoingia nchini kufanya kazi za msimu wa kilimo na uvuvi.

Mfumo huo ulizinduliwa jana jijini Mbeya kwenye Ofisi za Idara ya Uhamiaji na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ikibainishwa kuwa vibali hivyo vitakuwa vinatolewa kwa wageni hao ambao watakuwa wanakuja nchini kwa ajili ya shughuli za muda mfupi.

Mkuu wa Idara ya Uhamiaji Mkoa wa Mbeya, Kigongo Shile, aliyataja mataifa ambayo raia wake watanufaika na vibali hivyo kuwa ni Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Zambia.

Wengine ni raia wa Zambia na Msumbuji ambao watapatiwa vibali kwa ajili ya kushiriki kazi za msimu kama vile kuandaa mashamba, kulima, kupanda, kupalilia, kuvuna, uvuvi na kazi zingine zinazohusiana na sekta hizo.

Alisema lengo la serikali kuanzisha mfumo huo ni kuwatambua na kuwaratibu raia wa kigeni wanaokuja kufanya shughuli za msimu nchini na kuwezesha kampuni zinazotumia raia wa kigeni kwenye shughuli za msimu kuwatumia bila kificho.

Vilevile, alisema serikali inalenga kuzuia upotevu wa mapato ambayo yanapotea kutokana na wageni hao kuingia nchini na kufanya kazi bila kufuata taratibu za kisheria.

"Kibali hiki ni kwa ajili ya kuwasaidia hawa raia wa kigeni kufanya kazi nchini, lakini ili mtu akipate kibali hiki anatakiwa kuwa na nyaraka mbalimbali ikiwamo hati ya kusafiria, utambulisho wa mwenyeji wake na barua ya Ofisa Mtendaji wa Kata aliyofikia," alisema Kamanda Shile.

Alisema kwa mujibu wa Kanuni za Uhamiaji zilizoainishwa kwenye Tangazo la Serikali namba 657 la mwaka 2017 (GN.657) gharama za vibali hivyo zimegawanyika katika makundi mawili ambayo ni wageni wanaokuja kufanya kazi kwa watu binafsi na wanaokuja kufanya kazi kwenye kampuni.

Alisema kwa mgeni wageni wanaoingia nchini kwa ajili ya kufanya kazi kwenye kampuni, gharama yake ni Sh. 50,000 kwa muda wa miezi mitatu na Sh. 100,000 kwa wageni wanaokuja kufanya kazi kwa muda wa miezi sita.

Alisema kwa wageni wanaokuja kufanya kazi kwa watu binafsi, watatakiwa kulipa Sh. 30,000 kwa muda wa miezi mitatu na Sh. 60,000 kwa muda wa miezi sita.

Akizindua huduma hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Homera alisema aliwataka maofisa wa idara ya uhamiaji kuendelea kutoa elimu kwa wananchi ili wachangamkie fursa hiyo na waachane na kuajiri wahamiaji haramu.

Alisema vibali hivyo vitasaidia kuinua uchumi wa taifa kutokana na kuingiza fedha pamoja na kuongeza nguvukazi ya uzalishaji kwenye sekta hizo za kilimo na uvuvi pamoja na kuondokana na tatizo la wahamiaji haramu.

"Niwaombe tu wananchi waendelee kutembelea ofisi za uhamiaji ili wapate elimu kuhusu vibali hivi, tumeweka mifumo mizuri ambayo itatusaidia vibali hivi visitumike vibaya na wageni hao watakuwa na nafasi ya kuhuisha vibali hivyo kila vinapoisha muda wake kwa gharama zilizoainishwa," alisema Homera.

Alisema vibali hivyo havitawahusu wageni kutoka kwenye mataifa mengine ambayo ni nje ya yaliyoainishwa na kwamba wakiingia watahesabika ni wahamiaji haramu.



## ZIC yatoa vifaa tiba

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Bima Zanzibar (ZIC) katika kuadhimisha miaka 53 tangu kuanzishwa kwake, limeandaa matukio kadhaa likiwamo kutoa msaada wa vifaa tiba katika Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja, Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa Bima ya Kawaida wa ZIC, Jape Khamis, alisema mbali na msaada huo, shirika hilo pia limejipanga kutoa zawadi kwa wateja wake ambao watakata bima kupitia ofisi za kanda au kwa wakala wake.

Kuhusu kukabidhi vifaa tiba, Khamis alisema tukio hilo linatarajia kufanyika Juni 18 ambapo lengo lake ni kuunga mkono juhudi za serikali na wadau mbalimbali wakiwamo wateja wa shirika hilo katika kuboresha sekta ya afya visiwani humo.

"Kupitia wananchi hawa, ndipo biashara yetu inapofanikiwa na hivyo tuna wajibu wa kuchangia maendeleo ya nchi hii kupitia nyanja mbalimbali ikiwamo sekta ya afya.

"Matatizo sekta ya afya kwetu ni jambo la kipaumbele, kwa kuwa afya ndiyo msingi wa uchumi na uzalishaji mali na ni kichocheo kikuu cha maendeleo ya wananchi," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema shirika hilo limeandaa hafla maalum likilenga kukutana na wateja wake kwa ajili ya kujipongeza kwa pamoja, kupata mrejesho kutoka kwa wateja kuhusu huduma zake, kujadili fursa za biashara pamoja na kuzindua huduma mpya za bima zikiwamo huduma za Tour Operator Insurance, Travel Insurance pamoja na programu maalum ya mtandaoni kwa ajili ya huduma za shirika hilo.

"Kupitia App hii ya ZIC, wateja wetu wataweza kupata huduma zote za msingi tunazozitoa ikiwamo kukata bima pamoja na kujifunza mengi kuhusu huduma na shirika kwa ujumla kupitia simu zao za mkononi," alisema.

Alitoa wito kwa wadau na wateja wa shirika hilo kote nchini kuwaunga mkono katika maadhimisho hayo kwa kuendelea kutumia huduma za shirika hilo ikiwamo programu hiyo ya kimtandao ambayo inalenga kuwarahisishia upatikanaji wa huduma zake bila kutembelea ofisi za shirika hilo.

# Wanawake kuongezwa zaidi ngazi ya uamuzi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

UMOJA wa Vyama vya Siasa umepitisha maazimio ya kuwashirikisha wanawake katika kugombea nafasi mbalimbali za ngazi za uamuzi ndani ya vyama vya siasa.

Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa, Juma Ali Khatib, alibainisha hayo jana wakati wa mkutano wa kujadiliana namna bora ya kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi za uongozi na uamuzi uliofanyika Mjini Zanzibar.

Khatib alisema baraza la vyama vya siasa limeridhia utungwaji wa kanuni ya kifungu cha 6(a) na 6(b) cha Sheria ya Vyama vya Siasa ili kifanyiwe marekebisho na kuongeza makosa ya udhalilishaji wa kijinsia kuwa mojawapo ya mambo yatakayobatilisha sifa za mwanachama kuwa kiongozi wa chama.

Alisema Baraza la Vyama vya Siasa limeridhia mabadiliko katika sheria inayohusu uundwaji wa baraza la vyama vya siasa katika kifungu 21b(1) cha sheria ya vyama.

Alisema baraza hilo limeridhia mabadiliko katika sheria inayohusu uundwaji wa baraza la vyama vya siasa katika kifungu cha 21B (1) cha sheria hiyo ili idadi ya wajumbe wanawake kutoka kwenye vyama iongezeke.

Alisema ni lazima Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa isimamie utekelezaji wa namna ya kuwapata wanawake wenye sifa za kuingia katika baraza kwa kuwashirikisha wadau.

Mwenyekiti huyo alisema viongozi wengi wa vyama vya siasa hawapendi kumpa nafasi mwanamke katika kugombea kutokana na mfumo dume ulipo.

Khatib alisema kutokana na mazimio yaliyopitishwa na baraza hilo, sasa lazima kanuni na sheria zibadilike ili kumpa uwezo zaidi mwanamke kugombea nafasi katika vyama vya siasa.

Alisema pamoja na kuwapo kwa nafasi ndogo ya kugombea nafasi lakini bado wanawake wengi hawako tayari kuziomba

Naibu Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania bara, Christina Mndeme, alisema azimio la Baraza la Vyama vya Siasa Tanzania ni uamuzi sahihi katika kufikia malengo ya 50 kwa 50.

Alisema CCM imewapa nafasi wanawake katika vyombo vya uamuzi ikiwamo Bunge na Baraza la Wawakilishi kwa nafasi za viti maalum na majimbo ya uchaguzi.

Alisema bado kuna matatizo makubwa kwa baadhi ya vyama vya siasa kutokuwa na mfumo kama wa CCM na kueleza kuwa tamko hilo wanaamini litaleta mafanikio kwao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania, Lilian Liundi, alisema taasisi yake imeamua kuliunga mkono Baraza la Vyama vya Siasa kutokana na dhamira yake ya kuwashirikisha wanawake katika ngazi ya kugombea katika siasa.

Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa Tanzania, Mohammed Ally Ahmed, alisema vyama vilivyopatiwa usajili wa kudumu vimeshatoa mapendekezo yao na kuyakabidhi ofisi ya msajili ili kuyapeleka serikalini.

Alisema ofisi yao haina pingamizi kwa sababu ni daraja la kuunganisha taasisi za serikali.




Mkurugenzi wa Bima ya Kawaida wa Shirika la Bima Zanzibar (ZIC), Jape Khamis (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu mipango ya shirika hilo kuelekea maadhimisho ya miaka 53 tangu kuanzishwa. Wengine ni Ofisa Masoko na Uhusiano wa shirika hilo, Mohammed Shabani (kulia) na Ofisa Mauzo, Victoria Mwampogo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watumishi Ofisi ya Mtakwimu mbaroni tuhuma udanganyifu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) inawashikilia maofisa wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa tuhuma za kujipatia Sh. milioni 50.4 kwa njia ya udanganyifu.

Akizungumza jana na waandishi wa habari mjini hapa, Kamanda wa Mkoa wa Mjini Unguja wa Mamlaka hiyo, Bakari Hassan Mohammed, aliwataja watuhumiwa hao ni Issa Ramadhan (33), mkazi wa Michenzani ambaye ni Ofisa Ununuzi; na Fadhil Ali (40), mkazi wa Fuoni, Ofisa Takwimu.

Alisema Juni 10 mwaka huu, bila ya halali watuhumiwa hao walijipatia kiwango hicho cha fedha kwa njia ya udanganjifu jambo ambalo ni kinyume cha sheria.

Kamanda huyo alisema ZAECA inafanya kazi kubwa katika kuwatafuta wahalifu ambao kazi yao ni kuhujumu uchumi na kufanya kazi kwa kuendekeza rushwa.

Alisema hivi sasa kuna udanganyifu unaofanywa na baadhi wa watu kwa kujifanya maofisa ya ZAECA na huwapigia simu wananchi kuwa wanaitwa na mamlaka hiyo.

Alisema ZAECA ni taasisi kubwa na kwamba inapotaka kumwita mtu, hufanya hivyo kwa kumwandikia barua ya wito au kupiga simu kwa namba maalum inayotumiwa na mamlaka hiyo.

Aliwaomba wananchi wa Zanzibar kushirikiana na taasisi hiyo katika kuwabaini na kuwafichua wahalifu wa uhujumu wa uchumi na wala rushwa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NASSIRI ABDALLAH MOHAMED** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T914DCS** aina ya **TOYOTA PROBOX VAN**, yenye Chasis **No. NCP500062971**, Engine **No. PNZ4282605.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. **Taarifa ya polisi DOD/-DOD/RB/232403/2022.**

---

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA YA MBEYA**
**SHAURI NA.139 NA 138/2021**

**UWAMU SACCOS..........................MDAI**
**DHIDI YA**
**CHARLES JOHN ZIMBA...............MDAIWA**
**NEEMA MICHAEL MWAKISOLE.............................MDAIWA**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**KWA:**
**CHARLES JOHN ZIMBA NA NEEMA MICHAEL MWAKISOLE**
Fahamu kwamba UWAMU SACCOS AMEFUNGUA Shauri dhidi yenu katika Baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa tarehe **30/06/2022 saa2.30** asubuhi mbele ya Mh.T .Munzerere Mwenyekiti wa Baraza. Mnatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Mnaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria. Ofisi za baraza zipo ndani ya Saba saba Mbeya mjini.
Kumbuka Msipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo nyie kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa baraza hili leo tarehe 31/05/2022.

---

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA YA SONGWE**
**SHAURI NO.6/2022**
**ANYIGULILE M.MWASHILINDI:::::::::MDAI**
**DHIDI YA**
**DIANA C.MGALA:::::::::::::::MDAIWA**
**YAH:KUITWA SHAURINI**

**KWA:.**
**DIANA C.MGALA,**
Fahamu kwamba **ANYIGULILE M.MWASHILI**NDI amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa tarehe 17/06/2022 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh.T.Munzerere Mwenyekiti wa Baraza.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Songwe.
Unaamriwa kuhudhuria Mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisini za baraza zipo Mkoa was Songwe,wilaya ya Mbozi.
Kumbuka: Usipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/muhuri wa baraza hili leo tarehe 13/05/2022.

................................
**T.Munzerere**
**MWENYEKITI**
**13/05/2022**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**FERISTER CHANIKA** anatangaza kupotelewa na cheti cha chuo(ELEMENTARY AND PRACTICAL NURSING). Kilichotolewa na TOSAMAGANGA SCHOOL OF NURSING ASSISTANTS kwa mtihani wa mwaka 1985 katika chuo cha TOSAMAGANGA SCHOOL OF NURSING ASSISTANTS . Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **Taarifa ya Polisi namba IRI/IRI/RB/179874/2022.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Kihonda**
**Wilaya ya Morogoro**
**Mkoa Wa Morogoro**
**Usimamizi wa Mirathi Na...33..2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: LUCAS MWITA GAIN WA KIHONDA MBUYUNI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA: MERCY LUCAS MWITA**

**TANGAZO**

*(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)*

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 21 Mwezi 06 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

**Imetolewa Tarehe 14 Mwezi 06 Mwaka 2022**

**HAKIMU**


**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie: 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## RC: Watoto wasiosoma wanatumikishwa zaidi

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Dk. Batilda Burian, amesema watoto milioni 4.5 sawa na asilimia 28.8 wanatumikishwa katika kazi mbalimbali za kiuchumi.

Dk. Burian aliyasema hayo jana kwenye maadhimisho ya siku ya kupinga ajira na utumikishwaji watoto iliyofanyika wilayani Sikonge, mkoani Tabora.

Alisema utafiti uliofanywa na mradi Prosper Reset umebaini kuwa watoto wanaofanya kazi katika sekta za kilimo, misitu na uvuvi zinaajiri asilimia 92.1 ya watoto wote wanaojishughulisha na shughuli za kiuchumi.

Alisema utafiti huo umebainisha shughuli za kujisomea kwa watoto ni asilimia 15.5 na kati ya hao wavulana wanatumia muda mrefu zaidi kujisomea kwa asilimia 16.4 na wasichana hutumia asilimia 14.6.

Mkuu huyo wa mkoa aliongeza kuwa matokeo yameonyesha kuwa utumikishwaji wa watoto ni mkubwa kwa wasiosoma ikilinganishwa na wanaosoma.

Alisema utumikishwaji huo umeonesha kuwa ni mkubwa katika maeneo ya vijijini ikilinganishwa na mjini.

Dk. Batilda alisema utumikishwaji wa watoto bado ni tatizo kubwa kwa kuwa unaambatana na utoro kwa wanafunzi na mimba za ututoni.

Aliagiza kukomeshwa ajira za watoto mkoani hapo huku akitaka uwapo mpango kazi kutokomeza ukatili wa wanawake na watoto ngazi za vijiji, kata na wilaya zitekeleze kwa vitendo mipango yao kama zilivyoainishwa.

Vile vile, aliagiza kampuni za tumbaku kuendelee kupinga watoto kushiriki katika uzalishaji wa zao hilo na kuendelea utolewa elimu kwa wakulima kupitia miradi mbalimbali.

# Spika amwonya Waitara

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amemwonya Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara, kuacha dharau dhidi ya Bunge na aheshimu kanuni na taratibu za uendeshaji wa muhimili huo.

Aidha, Spika alitangaza msamaha kwa mbunge huyo ambaye amewahi kuwa Naibu Waziri na kumtaka asirudie tena kosa hilo.

"Kwa kuwa nilishaelekeza cha kufanya na niliielekeza serikali, haikubaliki kuvunjia heshima Bunge, kumvunjia heshima Spika. Pamoja na uzito wa makosa yake nampa onyo asirudie kudharau maamuzi ya Spika, na baada ya kumpa onyo hilo nimemsamehe," alisema.

Akizungumzia jambo hilo, Spika Tulia alisema mbunge huyo alihojiwa na gazeti moja (sio Nipashe), inayohoji na kupinga uhalali wa uamuzi niliotoa.

Alisema mbunge huyo alinukuliwa "Ni vigumu serikali inayotuhumiwa kutenda jambo fulani kwenda kujichunguza na badala yake Bunge lilipaswa kuunda kamati teule kwenda kuchunguza na taarifa kuwasilishwa kwake (bunge) si kama alivyofanya Spika."

"Hifadhi ya Serengeti ni ya serikali, sasa serikali inawezaje kujichunguza kwa kuwa serikali inalalamikiwa na Spika amewahi kuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ilitakiwa iundwe kamati teule ya bunge ikachunguze kisha taarifa iwasilishwe bungeni, ripoti ikija bungeni ijadiliwe na mapendekezo yawasilishwe serikalini, sasa serikali kujichunguza kuna shida," alisema.

Kwa mujibu wa Spika, maelezo ya mbunge huyo kusema serikali kujichunguza kuna shida kwa serikali kufanya uchunguzi inamaanisha serikali na vyombo vyake vyote vya uchunguzi kama polisi, TAKUKURU, Jeshi Usu na Usalama navyo vina shida jambo ambalo sio kweli."

Spika alisema kanuni za Bunge zinaeleza mbunge ambaye hataridhika na maamuzi ya Spika anatakiwa kuwasilisha malalamiko yake kwa Katibu wa Bunge kwa maandishi ili yafanyiwe kazi kwa mujibu wa kanuni na kwamba Mbunge huyo hakutaka kutumia utaratibu huo na badala yake kwenda kwenye vyombo vya habari.

"Maelezo ya Mwita dhidi ya uamuzi wangu yanakiuka sheria na kanuni zetu...kanuni inazuia mbunge kutoa maneno yanayovunja heshima ya Spika na kudhalilisha makusudi heshima ya Bunge, makosa aliyoyafanya yako kikanuni.

"Makosa yake yanajidhihirisha kwa kupuuza uamuzi au maelekezo ya Spika, kueleza kwamba Spika amewahi kuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali inashusha hadhi ya Spika kwamba Bunge linaongozwa na Spika mwanasheria, lakini hajui utaratibu," alisema.

Alisema; "kwa kuzingatia athari za kitendo alichokifanya kuvunja hadhi na haki ya Bunge, kwa kutumia mamlaka yangu kusimamia matumizi sahihi ya kanuni za Bunge mtu mwenye afya ya akili alipaswa kuelewa maana ya maelezo niliyo yatoa."

"Kanuni zetu ziko wazi kabisa adhabu gani anastahili mtu wa namna hii ambaye ni utovu mkubwa wa nidhamu," alisisitiza.



Dereva wa basi aina ya Scania Irizar lenye namba za usajili AJE 6880 la kampuni ya Royar Luxury, Gregor Lumato, akizungumza na waandishi wa habari, baada ya basi hilo kuwasili katika kituo cha mabasi cha John Magufuli, Mbezi Mwisho, mkoani Dar es Salaam juzi kutoka nchini Afrika Kusini, wakati wakizindua rasmi safari zake kati ya Dar – Zambia hadi Afrika Kusini. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Serikali yaonya wanaosafirisha mazao bila kibali

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imetoa onyo kali kwa wafanyabiashara watakaosafirisha mazao bila kibali, mali zao zitakamatwa na hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Onyo hilo lilitolewa jana na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapo, baada ya malori zaidi ya 30 ya mazao kukwama kwenye mpaka wa Namanga, jijini Arusha kwa kutokuwa na vibali vya usafirishaji.

Alisema hakuna sababu ya wafanyabiashara kutumia njia za panya kusafirisha mazao kupeleka sehemu yoyote kwa sababu serikali haijafunga mipaka ya kufanya biashara hiyo.

Aliwataka kufuata taratibu na sheria za usafirishaji wa mazao.

"Tunakwenda kusaidia malori haya yapate vibali ili waendelee na safari, lakini suala hili lisijirudie tena, kila mfanyabiashara anatakiwa kuchukua kibali kabla ya kupeleka biashara na vinatolewa mtandaoni ili kupunguza msongamano mipakani," alisema Bashe.

Alisema mfanyabiashara yeyote atakayebainika anasafirisha mazao kwa njia za panya atahesabika kama mhalifu kwa sababu atakuwa amekiuka taratibu zilizopangwa na serikali za usafirishaji mazao. Alikemea tabia ya wafanyabiashara kwenda vijijini kununua mazao kabla ya kuchukua vibali na kuanza safari kuelekea mipakani.

"Akifika mpakani ndiyo anaanza kutafuta kibali hiyo haikubaliki na wala serikali haitavumilia suala hilo kwa yule atakayebainika kafanya hivyo," alisema.

Alisema serikali haizuii watu kufanya biashara kinachotakiwa ni watu wafuate taratibu za ufanyaji biashara zilivyoelekezwa na mamlaka husika ili wawe salama katika biashara hiyo.

Pia kama nchi wanapotoa vibali vya nje kwa sababu ya kutaka kuangalia na kuona kama kweli mazao hayo yanatoka Tanzania na yanakwenda Kenya au nchi nyingine, ili kesho na keshokutwa asije

akatokea mtu akaharibu soko la mazao ya Tanzania katika masoko makubwa ambayo nchi inayategemea.

"Tunaomba utaratibu wa kuhakikisha wafanyabiashara wanapata vibali, lakini wahakikishe wanapata certificate (cheti) cha ukaguzi wa afya ya mimea ni lazima uwe nayo," alisema Bashe.

Alisema kumekuwa na tabia ya wafanyabiashara kuchukua vibali vya usafirishaji mizigo na akifika mpakani anakuta mzigo umezidi ndio anaanza kutaka abadilishiwe kibali kilingane na mzigo alioubeba.

"Hilo suala halikubaliki hata kidogo kama nchi tunaruhusu watu kuuza na kununua hivyo wafanyabiashara fuateni taratibu tunazopanga. Wapo wanaotorosha mali kwa njia za panya, sijui kwanini wanafanya hivyo ilhali serikali haiwachaji chochote katika usafirishaji zaidi ya vibali ambavyo vinatakiwa mfanyabiashara awe navyo," alisema.

# GEITA GOLD FC YATEMBELEA MIRADI INAYOFADHILIWA GGML

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya mpira wa miguu ya Geita Gold FC, inayodhaminiwa na Kampuni ya GGML, imetembelea miradi ya jamii inayofadhiliwa na kampuni hiyo kupitia mpango wake wa huduma kwa jamii.

**Akizungumza wakati wa ziara ya timu hiyo, Meneja Mwandamizi anayehusika na Ubia GGML, Manace Ndoroma, amesema pamoja na kutoa udhamini wa shilingi milioni 500 kwa timu hiyo, wameamua kuikaribisha timu hiyo kuona uwekezaji unaofanywa na kampuni hiyo katika jamii ya Geita.**

"Tumefarijika sana kuwa wadhamini wakuu wa timu ya Geita Gold Football Club kwa sababu jitihada zao za kupanda katika msimamo wa Ligi Kuu, zimeongeza chachu ya michezo kwa mkoa wetu wa Geita. Timu hii sasa imekuwa balozi wetu mzuri anayetutangaza sisi GGML, Mji wa Geita na mkoa wetu kwa ujumla," alisema Ndoroma.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Geita Gold, Simon Shija, yeye aliipongeza Kampuni ya GGML kwa kuendelea kuinufaisha jamii ya Geita kupitia miradi mbalimbali ya maendeleo.

"Watu wengi wanaisifia timu yetu kwa kufanya vizuri katika msimamo wa ligi. Lakini siri ya mafanikio yetu ni pamoja na kushikwa mkono na wadau mbalimbali wakiwamo GGML ambao pamoja na kutupatia udhamini mkuu, wanatujengea uwanja wa mpira wa kisasa Mjini Geita. Ni matumaini yetu kuwa hata tutakapokuwa tunacheza mechi ngumu dhidi ya timu za Simba, Yanga hapa mjini Geita, mashabiki wetu wa ndani na nje ya Geita watafurahia na kutushangilia kutokana na uwekezaji wa GGML ndani ya mji huu (Geita). Pia tunatoa rai kwa wadhamini wengine waendelee kutushika mkono, kwani timu yetu inatamani kuendelea kufanya vizuri zaidi kwa msimu ujao," alisema Shija.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Geita, Lee Joshua, ameipongeza GGML kwa kuendelea kuwekeza kwenye jamii katika halmashauri yake kwa wakati, hatua inayorahisisha utekelezaji wa miradi mingi ya maendeleo yenye tija katika jamii.

"Halmashauri yetu ya Mji Geita, imekuwa mnufaika wa uwekezaji mkubwa kwenye miradi ya jamii. Mojawapo ya matunda ya uwekezaji huo ni utekelezaji wa miradi mikubwa ya ujenzi wa soko la dhahabu, soko la Katundu, barabara za lami pamoja na Kituo cha Uwekezaji cha EPZA: miradi ambayo timu yetu ya mpira ya Geita Gold Football Club imetembelea leo. Pia, tunafurahia kutembelea miradi hii pamoja na timu yetu ya mpira ambayo kwa kiasi kikubwa imeweza kutangaza vivutio vya Mkoa wa Geita, zikiwamo sehemu za utalii," alisema Lee.

Katika ziara hiyo, timu ya Geita Gold Football Club ilipata pia fursa ya kuwafariji na kupata nao chakula cha mchana watoto yatima wa Kituo cha Moyo wa Huruma kinachofadhiliwa na GGML kupitia mradi wake wa Kili Challenge.

GGML imekuwa kinara wa uwekezaji kwenye jamii tangu kuanzishwa kwake mwaka 2000 ambapo vipaumbele vikuu vimekuwa ni miradi ya elimu, afya, maji, barabara, miradi ya kukuza kipato na mingine mingi ya kijamii ili kuhakikisha jamii mwenyeji inapata maisha bora. Mapema mwaka huu, GGML iliibuka mshindi wa jumla katika kampuni zinazofanya vizuri kwenye sekta ya madini nchini Tanzania kwa mwaka 2020/2021 baada ya kunyakua tuzo katika vipengele vya uwajibikaji wa kampuni kwa jamii, mazingira, usalama, mlipaji bora wa mapato (kodi) na uendelezaji wazawa.



Kocha Mkuu wa Klabu ya Geita Gold FC, Fred Felix 'Minziro' (kulia), akikabidhiwa mpira na Meneja Mwandamizi wa masuala ya Ubia wa GGML, Manace Ndoroma, baada ya kutembelea miradi mbalimbali inayotekelezwa na GGML kupitia mpango wa uwajibika wa kampuni kwa jamii (CSR). **NA MPIGAPICHA WETU**

# New Generation yapoteza ubingwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya New Generation imeendelea kupoteza matumaini ya kuwa bingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Zanzibar baada ya juzi kupokea kichapo cha bao 1-0 dhidi ya UMZ katika mwendelezo wa ligi hiyo.

Kwa matokeo hayo New Generation imeendelea kusota nafasi ya pili ikiwa na alama 40 katika msimamo wa ligi hiyo huku wapinzani wao wakuu, Warriors Queens, wakiendelea kutamba kileleni mwa ligi hiyo kwa pointi zao 46 wakati UMZ yenyewe tayari imemaliza mechi za msimu huu ikiwa katika nafasi tatu.

New Generation ambao ndio wababe kwa timu za Wanawake Zanzibar, msimu huu haikufanya vizuri ikilinganishwa na msimu uliopita.

Akizungumza na gazeti hilo Katibu wa timu hiyo Abdu Seif Ali, alisema kufanya vibaya kwa timu hiyo kumetokana na wachezaji wake kujiamini kupita kiasi kwa kujiona wa ndio timu bora mara zote.

Alisema wachezaji hawakuwa na hofu ya mchezo unaokuja mbele yao kwakuwa tayari wao walijijengea kuwa watapata alama tatu kila wanaposhuka dimbani.

Katibu huyo alisema tatizo hilo ndilo limesababisha kupata matokeo wasiyoyatarajia ikiwamo kufungwa michezo miwili na kutoka sare mchezo mmoja jambo ambalo lililosababisha kupoteza matumaini ya ubingwa.

Ligi Kuu ya Wanawake Zanzibar imebakisha michezo nane kumaliza ligi hiyo kwa msimu huu ambapo michezo hiyo itachezwa Kisiwani Pemba.

Katika michezo hiyo nane, Warriors Queens imebakiza mechi mbili, hivyo inahitaji alama moja tu ili kutawazwa mabingwa wa ligi hiyo msimu huu, wakati New Generation, Future Queens na Dunga Queens nazo kila moja ikibakiwa na mechi mbili.

# *Mtibwa Sugar yatoa siri ushindi Ruvu Shooting*

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la Ufundi la Klabu ya Mtibwa Sugar, limesema siri ya timu yao kupata pointi tatu katika mchezo dhidi ya Ruvu Shooting ni kutokana na mapumziko marefu waliyopata kwa kupisha majukumu ya timu za taifa.

Akizungumza na gazeti la Nipashe jana, Kocha Msaidizi wa klabu hiyo, Awadhi Juma, alisema mapumziko hayo yaliwasaidia wachezaji kupumzisha akili pamoja na miili yao, hivyo kurejea wakiwa na nguvu mpya.

"Mapumziko yametusaidia kuandaa vizuri wachezaji wetu ikiwamo kucheza michezo ya kirafiki ambayo imezidi kutuweka mahali pazuri," alisema Juma.

Aliwapongeza wachezaji wake kutokana na kazi kubwa waliyoifanya katika mchezo huo ambao ulikuwa na ushindani mkubwa.

Alisema katika mchezo huo amebaini mapungufu madogo ya kiufundi ambayo ameahidi watakwenda kuyafanyia kazi haraka iwezekanavyo.

Juma alisema kabla ya mchezo huo kila mchezaji alihitaji ushindi ili wajitoe sehemu jambo ambalo wamefanikiwa na kujiweka pazuri.

Matokeo hayo yameifanya Mtibwa Sugar kushika nafasi ya 11 kwenye msimamo wa ligi hiyo, ikiwa na alama 31 sawa na Dodoma Jiji iliyoko nyuma yao baada ya timu hizo kila moja kushuka dimbani mara 27.

## ZISIKUPITE

### DE JONG NA UNITED

MANCHESTER United imeanza mazungumzo na Barcelona kwa ajili ya usajili wa kiungo wa Uholanzi, Frenkie de Jong, 25, lakini hawatataka kulipa fedha kubwa kupita kiasi wakati huu klabu hiyo ya Hispania ikitaka pauni milioni 85.7. ***(Manchester Evening News)***

### RICHARLISON ATAKIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inataka kumsajili mshambuliaji wa Everton na Brazil, Richarlison, 25, huku Toffees hao wakitaka ada ya pauni milioni 50 kwa ajili ya nyota huyo wa Brazil. ***(Telegraph)***

### LIVER, CITY KWA GAVI

LIVERPOOL na Manchester City wanamfuatilia kiungo wa Barcelona na Hispania, Gavi, 17 na ada ya uhamisho wake kwenye mkataba imefikia pauni milioni 85.7. ***(Marca)***

### NKUNKU BEI JUU

KLABU ya RB Leipzig inamuuza kwa ada ya pauni milioni 100 mshambuliaji wake Mfaransa, Christopher Nkunku, 24, huku Manchester United, Arsenal na Paris St-Germain zikionyesha nia ya kumtaka. ***(Independent)***

### NEWCASTLE WAMTEMA BOTMAN

NEWCASTLE United inatarajia kusaka mchezaji mwingine baada ya Lille kupandisha dau la mlinzi, Sven Botman, 22, kutoka pauni milioni 30 mpaka milioni 36. ***(Telegraph)***

### LENO ANUKIA FULHAM

KLABU ya Fulham inamtaka kipa wa Arsenal na Ujerumani, Bernd Leno, 30. ***(Evening Standard)***

### PHILLIPS AWINDWA CITY

KLABU ya Manchester City inataka kumsajili nyota wa Leeds United na England, Kalvin Phillips, 26, huku pia akiwindwa na klabu kadhaa. ***(Times)***

### SANUSI ASAKWA BRIGHTON

KLABU ya Brighton inamsaka mlinzi wa kushoto wa Porto na Nigeria, Zaidu Sanusi , 25, katika uhamisho utakaomruhusu nyota wa kimataifa wa Hispania, Marc Cucurella mwenye umri wa miaka 23 kujiunga na Manchester City. ***(Daily Star)***

### HEATON NA MIDDLESBROUGH

KLABU ya Middlesbrough inamtaka kwa mkopo kipa wa Manchester United na England, Tom Heaton, 36, na kiungo wa Leicester City, Hamza Choudhury mwenye umri wa miaka 24. ***(Northern Echo)***


### ROCA HUYOOO LEEDS

LEEDS United ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha uhamisho wa kiungo wa Bayern Munich, Marc Roca, 25. ***(90min)***

### PARROTT AGOMBEWA ENGLAND

SWANSEA City, Middlesbrough, Preston na QPR, zote zinamuwania kwa mkopo mshambuliaji wa Tottenham Hotspur na Jamhuri ya Ireland, Troy Parrott, 20, kwa ajili ya msimu ujao wa 2022-23. ***(Football. London)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND AFUNGUKA MAHREZ ALIVYOMSHAWISHI KUTUA CITY

●●● Aliniambia nije City, alikuwa sahihi kuhusu hilo, alisema baadhi ya mambo mazuri kuhusu klabu...

**MANCHESTER,** England

ERLING Haaland amefichua kwamba, Riyad Mahrez alimwambia asaini Manchester City mwaka jana, na mshambuliaji huyo pia anasubiria kwa hamu kucheza na Phil Foden.

**Mabingwa hao wa Ligi Kuu England walitangaza Mei 10, mwaka huu kufikia makubaliano ya kumsajili Haaland kutoka Borussia Dortmund kwa ada ya euro milioni 60 na juzi Jumatatu alikamilisha rasmi usajili huo.**

Haaland sasa amesaini rasmi mkataba wa miaka mitano wa kucheza hapo kwenye Uwanja wa Etihad, ambapo Julai Mosi ndio atakuwa mchezaji rasmi wa Man City.

Haaland alifunga mabao 86 katika michezo 89 ya Dortmund tangu alipojiunga kutoka Salzburg Januari 2020, akifunga bao kila baada ya dakika 84 kwenye mashindano yote.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, alipigwa picha akiwa na Mahrez wakiwa likizo nchini Ugiriki mwaka 2021, na Haaland aliiambia tovuti rasmi ya City kwamba, mchezaji huyo wa kimataifa wa Algeria alikuwa amezungumza naye kuhusu kuhamia Manchester wakati huo.

"Aliniambia nije City!" Alisema katika mahojiano hayo yaliyochapishwa Jumatatu.

"Alikuwa sahihi kuhusu hilo. Alisema baadhi ya mambo mazuri kuhusu klabu."

Haaland pia alionyesha kufurahishwa kwake na matarajio ya kuungana na mchezaji mwingine mchanga, Foden. Mchezaji huyo wa kimataifa wa England alitoa asisti 11 katika michezo 45 katika mashindano yote kwa City msimu uliopita, huku akitengeneza nafasi 63.

"Nimekuwa nikitazama mechi nyingi za Man City kwa muda mrefu niwezavyo kukumbuka. Bila shaka, basi pia nilimtazama Phil na ni mchezaji wa ajabu," alisema Haaland.

"Bado ni kipaji kwa sababu bado ni mdogo, lakini ni mchezaji wa ajabu. Ana nafasi kubwa sana ya kuimarika zaidi."

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,006,4

MECHI KALI
AZAM
VERSUS
MBEYA KWANZA FC
1 | 1.82
X | 3.10
2 | 4.90

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# SOUTHGATE AWAONYA WACHEZAJI MAN UTD

**LONDON,** England

KOCHA wa Timu ya Taifa ya England, Gareth Southgate amesema wachezaji wa Manchester United ambao hawako katika kikosi hicho wana "mengi ya kufanya" ili wapate nafasi kwenye Kombe la Dunia 2022 nchini Qatar.


Wakati beki Luke Shaw akiwa majeruhi, Marcus Rashford na Jadon Sancho hawajachaguliwa kutokana na kiwango kibovu, na hivyo kumuacha Harry Maguire kuwa mchezaji pekee wa United kwenye kikosi ambacho jana Jumanne kilitarajiwa kucheza na Hungary kwenye Ligi ya Mataifa ya Ulaya.

Rashford na Sancho wamekuwa hawapewi nafasi tangu England ilipofungwa na Italia kwenye fainali ya Euro 2020 mwaka jana, lakini Southgate alisema mwezi uliopita bado walikuwa na mechi za kutosha za klabu kuonyesha ubora wao na kubadili mawazo yake kabla ya Kombe la Dunia, Novemba.

Washambuliaji wote wawili walikosekana kwenye mechi tatu za mwisho za United za Ligi Kuu msimu huu, huku klabu hiyo ikimaliza nafasi ya sita, na kukosa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Alipoulizwa kama wachezaji wa United watakuwa na hali mpya katika msimu ujao bila ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya, Southgate aliwaambia waandishi wa habari: "Jambo ni moja tu. Wana mengi ya kufanya ili kurejea kikosini.





## Arsenal yabeba straika Sao Paulo

**LONDON,** England

ARSENAL wamemsajili mshambuliaji kinda, Marquinhos kutoka Sao Paulo kwa mkataba wa muda mrefu.

Marquinhos mwenye umri wa miaka 19, mchezaji wa kimataifa wa Brazil, alicheza mechi 33 na Sao Paulo na kushinda Kombe la Compeonato Paulista mwaka 2021.

"Tunafuraha kukamilisha uhamisho huo na Sao Paulo, kwani Marquinhos alikuwa mchezaji ambaye tulikuwa tukimtazama kwa muda," alisema Mkurugenzi wa Ufundi wa Arsenal, Edu.

"Akiwa na umri wa miaka 19, bado ni mdogo sana, kwa hiyo ni mchezaji wa siku zijazo.

"Tunamtarajia kwa hamu Marquinhos kuungana nasi kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya, kutengeneza nyumba yake mpya, na kuendelea kukua na kuendelea nasi."

ESPN iliripoti mwezi uliopita kwamba, dili hilo lingekuwa na thamani ya euro milioni 3.5 na kwamba klabu hizo mbili zilikubali ada baada ya Marquinhos kukataa ofa nyingi za mkataba mpya kwa klabu hiyo ya Brazil na vyanzo vilidai kuwa Arsenal walifanya haraka kupata makubaliano ya bei iliyopunguzwa.

Marquinhos ni mshambuliaji anayetumia mguu wa kushoto pia anaweza kucheza kama winga, lakini anatazamwa na Arsenal kama tegemeo la baadaye badala ya kusajiliwa mara moja katika kikosi cha kwanza.

## HABARI MICHEZO


442,235/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 18/06/22 | 20:00 | Enppi Club vs Coca Cola | 3.47 | 2.92 | 2.28 |
| 02. 18/06/22 | 21:30 | Gimnasia Mendoza vs Deportivo Maipu | 2.28 | 2.78 | 3.68 |
| 03. 18/06/22 | 22:00 | Londrina PR vs Vasco da Gama | 3.26 | 2.86 | 2.42 |
| 04. 18/06/22 | 22:00 | Seattle Sounders vs Los Angeles FC | 2.30 | 3.53 | 2.97 |
| 05. 19/06/22 | 00:00 | Arsenal Sarandi vs Talleres | 2.60 | 3.10 | 2.90 |
| 06. 19/06/22 | 00:30 | Nautico PE vs Sport Recife | 2.73 | 2.97 | 2.73 |
| 07. 19/06/22 | 01:00 | Cuiaba MT vs Ceara CE | 2.65 | 3.10 | 2.75 |
| 08. 19/06/22 | 01:10 | Almirante Brown vs Deportivo Moron | 2.44 | 2.76 | 3.36 |
| 09. 19/06/22 | 01:45 | Sportivo Ameliano vs Nacional Asuncion | 2.77 | 3.12 | 2.57 |
| 10. 19/06/22 | 02:30 | Sarmiento vs Patronato Parana | 2.58 | 3.18 | 2.88 |
| 11. 19/06/22 | 03:00 | Chicago Fire vs DC United | 2.21 | 3.43 | 3.22 |
| 12. 19/06/22 | 13:30 | Suwon Samsung vs FC Seoul | 2.69 | 3.09 | 2.74 |
| 13. 19/06/22 | 17:00 | Guarani SP vs CSA AL | 2.42 | 2.97 | 3.12 |
| 14. 19/06/22 | 19:00 | Jerv vs Ham-Kam | 2.88 | 3.33 | 2.39 |
| 15. 19/06/22 | 21:00 | Aalesunds vs Valerenga | 2.46 | 3.39 | 2.74 |
| 16. 19/06/22 | 21:00 | Gimnasia Jujuy vs Temperley | 2.33 | 2.72 | 3.66 |
| 17. 19/06/22 | 22:00 | Tenerife vs Girona | 2.44 | 3.08 | 3.03 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 15/06/2022

| MUDAVV | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 1339 | Wuhan Zall vs Wuhan Three Towns FC | 5.86 | 3.91 | 1.48 |
| 14:30 | 3843 | Guangzhou RF vs Henan Jianye | 9.63 | 4.82 | 1.27 |
| 15:00 | 1885 | Independiente Reserve vs Argentinos Juniors Reserve | 3.40 | 3.06 | 2.09 |
| 15:00 | 1955 | Velez Sarsfield Reserve vs Racing Club Reserve | 1.93 | 3.29 | 3.58 |
| 15:00 | 3507 | Zhfk Yenisey Krasnoyarsk W vs FC Zenit Saint Petersburg W | 10.75 | 4.20 | 1.30 |
| 16:00 | 1725 | Australia U23 vs Saudi Arabia U23 | 3.19 | 2.65 | 2.44 |
| 16:00 | 2861 | Dire Dawa Kenema FC vs Hawassa Kenema SC | 3.55 | 2.85 | 2.24 |
| 17:00 | 1795 | FC Samtredia vs Merani Martvili | 3.38 | 3.48 | 1.93 |
| 17:00 | 2432 | CA Aldosivi Reserve vs Patronato Reserve | 2.28 | 3.23 | 2.84 |
| 17:00 | 2747 | WIT Georgia vs Gareji | 2.03 | 3.34 | 3.24 |
| 17:00 | 3469 | Newells Old Boys vs CA Talleres de Cordoba Reserve | 2.29 | 3.25 | 2.81 |
| 17:00 | 5085 | FC Spaeri vs Metalurgi R | 1.95 | 3.58 | 3.24 |
| 17:00 | 5228 | Gimnasia de la Plata Reserve vs CA Platense | 2.06 | 3.44 | 3.10 |
| 17:00 | 5430 | CD Godoy Cruz vs Rosario Central Reserve | 4.10 | 3.60 | 1.80 |
| 18:00 | 4180 | Recanatese vs FC Giugliano 1928 | 2.65 | 3.25 | 2.50 |
| 18:30 | 1973 | MKS Piast Zmigrod vs Zaglebie II Lubin | 3.49 | 3.83 | 1.81 |
| 18:30 | 2146 | Miedz II vs Foto Higiena Gac | 1.35 | 5.10 | 6.08 |
| 18:30 | 2278 | Lahden Reipas vs Keski Uusimaa | 1.34 | 5.08 | 6.44 |
| 18:30 | 2482 | MKS Odra Wodzislaw Slaski vs Polonia Bytom SA | 3.68 | 3.63 | 1.81 |
| 18:30 | 2514 | LKS Goczalkowice-Zdroj vs MKS Kluczbork | 2.20 | 3.20 | 3.01 |
| 18:30 | 2736 | Azam vs Mbeya Kwanza FC | 1.75 | 3.14 | 4.80 |
| 18:30 | 2803 | Mkp Carina Gubin vs Pniowek Pawlowice Slaskie | 2.37 | 3.13 | 2.79 |
| 18:30 | 4284 | Warta Gorzow Wielkopolski vs KS Sleza Wroclaw | 3.84 | 3.69 | 1.76 |
| 18:30 | 5412 | Gornik Zabrze II vs Gwarek Tarnowskie Gory | 2.05 | 3.43 | 3.13 |
| 18:30 | 5763 | FC KTP vs IF Gnistan | 2.19 | 3.35 | 2.91 |
| 19:00 | 1930 | Ittihad Tanger vs FUS Rabat | 2.36 | 2.70 | 3.55 |
| 19:00 | 3563 | PK-35 vs Salpa Salo | 1.42 | 4.51 | 5.69 |
| 19:00 | 4517 | Uzbekistan U23 vs Japan U23 | 2.95 | 2.90 | 2.40 |
| 20:00 | 3517 | Korsnas IF FK vs Kvarnsvedens IK | 2.16 | 3.43 | 2.89 |
| 20:00 | 4753 | Barracas Central vs Union Santa Fe | 2.90 | 3.00 | 2.37 |
| 20:00 | 5869 | Frigg vs Skeid Fotball | 4.62 | 4.32 | 1.53 |
| 21:00 | 1391 | Mirassol FC U20 vs Votuporanguense SP U20 | 1.26 | 5.30 | 8.64 |
| 21:00 | 1794 | Atletica Internacional De Limeira U20 vs Comercial Tiete FC SP U20 | 1.36 | 4.81 | 6.48 |
| 21:00 | 3236 | Ibrachina FC SP U20 vs Portuguesa Desportos SP U20 | 1.80 | 3.49 | 3.88 |
| 21:00 | 3360 | Vestmannaeyjar vs Vikingur Reykjavik | 5.33 | 4.14 | 1.49 |
| 21:00 | 3824 | Ferroviaria SP U20 vs Taquaritinga SP U20 | 1.31 | 5.30 | 6.87 |
| 21:00 | 3948 | Tanabi EC SP U20 vs America FC SP | 1.26 | 5.60 | 9.60 |
| 22:00 | 2471 | Al Ahly Cairo vs Eastern Company SC | 1.14 | 7.05 | 18.14 |
| 22:15 | 4176 | KH Hlidarendi vs IH Hafnarfjordur | 1.92 | 4.40 | 2.83 |
| 22:15 | 5321 | KR Reykjavik vs IA Akranes | 1.30 | 4.94 | 7.70 |
| 22:30 | 3240 | Atletico Tucuman vs Lanus | 2.46 | 3.10 | 2.70 |
| 22:30 | 5154 | Banfield vs Central Cordoba | 2.12 | 3.09 | 3.29 |

ALHAMISI - 16/06/2022

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 01:00 | 2773 | Bragantino SP vs Coritiba | 1.72 | 3.38 | 4.51 |
| 01:00 | 3487 | Colon Santa Fe vs River Plate | 3.73 | 3.39 | 1.86 |
| 01:00 | 4396 | Ceara CE vs Atletico Mineiro | 3.28 | 3.14 | 2.10 |
| 02:00 | 4071 | Atletico Bucaramanga vs Millonarios FC | 3.47 | 3.08 | 2.05 |
| 02:30 | 1420 | Goias vs Internacional | 2.94 | 2.94 | 2.38 |
| 02:30 | 1563 | Flamengo vs Cuiaba MT | 1.29 | 4.72 | 8.86 |
| 02:30 | 5160 | New England vs Orlando City | 1.69 | 3.99 | 4.60 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.




# MPOLE HANA PRESHA NA MAYELE MBIO ZA KIATU

Na Saada Akida

HUKU akiwa kileleni mwa orodha ya wafungaji bora Ligi Kuu Bara, mshambuliaji wa Geita Gold FC, George Mpole, amesema hana presha na malengo yake ya kumaliza msimu akiwa kinara wa mabao na pia hana hofu juu ya kasi ya uchekaji na nyavu wa mpinzani wake wa karibu, straika wa Yanga, Fiston Mayele.

Mpole juzi alifunga bao lake la 15 msimu huu, hivyo kumpita Mayele mwenye mabao 14, kabla ya leo kuiongoza safu ya ushambuliaji ya Yanga dhidi ya Coastal Union katika mechi itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Mpole alisema kazi yake kubwa ni kuhakikisha anatumia nafasi nzuri atakazozipata kufunga bao ili kusaidia timu yake kufikia malengo yao ya kumaliza wakiwa nafasi ya tatu katika msimamo wa ligi hiyo.**

Alisema hana wasiwasi na Mayele katika kuwania kiatu cha ufungaji bora maana yuko tayari kwa ajili ya mapambano hayo ili kutimiza malengo aliyojiwekea.

"Siangalii Mayele anafanya nini zaidi, kwa sababu kila mtu na malengo yake, nimejiandaa kisaikolojia kupambana kwa ajili ya malengo yangu niliyojiwekea mwanzoni mwa msimu kuwa mfungaji bora kwa msimu huu," alisema.

Alisema anapambana kuhakikisha anafikia malengo kwa kutumia nafasi anazozipata ili kufunga katika michezo iliyosalia ya Ligi Kuu kufikia tamati pasipo kuangalia anachokifanya Mayele.

Baada ya juzi kupata ushindi wa mabao 2-0 nyumbani dhidi ya Dodoma Jiji FC, matokeo hayo yameifanya Geita Gold kupanda hadi nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo kabla ya mechi za jana.



George Mpole (jezi namba 9), akipongezwa na wachezaji wenzake wa Geita Gold FC, baada ya kuifungia timu yake bao la pili wakati ikishinda 2-0 dhidi ya Dodoma Jiji FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Nyankumbu mjini Geita juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Namungo yasaka pointi kurejea kimataifa*

Na Adam Fungamwango

WAKATI kesho ikitarajia kucheza dhidi ya Polisi Tanzania kwenye uwanja wake wa nyumbani, Ilulu mkoani Lindi, Kocha Msaidizi wa Namungo FC, Jamhuri Kihwelo 'Julio' amesema wana mpango mkakati wa kuzisaka pointi 12, ambazo zitapatikana kwa kushinda mechi zote nne za Ligi Kuu zilizobaki, ili kuirejea tena kwenye michuano ya kimataifa.

Akizungumza jana kuelekea kwenye mechi hiyo, Julio alisema lengo lao ni kushinda mechi hiyo na sababu kubwa hasa ni kuisaka nafasi ya tatu, ili kuweza kurejea kwenye michuano ya kimataifa.

"Tunataka kushinda mechi zote nne zilizobaki, kwa sababu tukifanya hivyo tutapata pointi 12 ambazo zitatupa mwanga na kuona mwisho wa siku tutakaa wapi. Tunataka nafasi ambayo itaturudisha kwenye mechi za kimataifa, hasa ya tatu, najua mechi itakuwa ngumu sana kwa sababu hakuna asiyefahamu kuwa Polisi Tanzania ni timu nzuri pamoja na kwamba tunacheza nyumbani, lakini haitokuwa rahisi, ni lazima tupambane kwenye mechi hii na zilizobaki," alisema.

Namungo mpaka sasa inashika nafasi ya nne kwa pointi 37, na iwapo itashinda kesho itakwea hadi nafasi ya tatu na kufikisha alama 40, ikiiacha Geita Gold ambayo ina pointi 39.

Msimu uliopita Namungo ilicheza Kombe la Shirikisho, ikifanya vizuri kwenye mechi za mwanzo hadi kufanikiwa kutinga hatua ya makundi, ingawa haikufanya vema kwenye hatua hiyo.

Iwapo Yanga itatwaa ubingwa wa Kombe la FA, timu zitakazoshika nafasi ya tatu na ya nne kwenye Ligi Kuu zitacheza Kombe la Shirikisho Afrika, lakini kama Coastal Union itatwaa ubingwa huo itakwenda kucheza michuano hiyo, hivyo kuwa nafasi ya nne kwenye Ligi Kuu, badala yake ni mshindi wa tatu tu ndiye atakayecheza Shirikisho.

Michezo
Jumatano Juni 15, 2022
Nipashe



Haaland afunguka Mahrez alivyomshawishi UKURASA 21

# Yanga yapania ubingwa leo

## Nabi atangaza kuwakosa mastaa watatu, Coastal yatamba, huku Azam nao wakieleza...

**Na Saada Akida**

LIGI Kuu Tanzania Bara mzunguko wa pili utaendelea leo kwa nyasi za viwanja viwili kuwaka moto, ambapo Yanga itakuwa mwenyeji wa Coastal Union ya Tanga katika Uwanja wa Benjamin Mkapa utakaopigwa saa 2:00 usiku Dar es Salaam wakati Azam FC ikiwakaribisha Mbeya Kwanza, kwenye Dimba la Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam mechi ikipigwa saa 12:30 jioni.

**Katika michezo hiyo miwili, timu zote zinahitaji matokeo mazuri kwa malengo tofauti, kwa upande wa Yanga inahitaji pointi tatu ili kutangaza rasmi ubingwa wa ligi hiyo kwa msimu huu wakati Coastal Unioni ushindi kwao ukiongeza matumaini ya mbio za kumaliza nafasi nne za juu.**

Coastal Union ambao wako nafasi ya sita kwa alama 34 iko katika vita vya kutafuta pointi ili kumaliza ligi hiyo katika nafasi ya nne kutokana na waliopo juu yake kupishana alama mbili hadi tatu.

Azam FC inayoshika nafasi ya tano inahitaji matokeo mazuri ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kumaliza nafasi ya nne kwa kudhamiria kumfunga Mbeya Kwanza ambao nao wanahitaji kujiondoa mkiani mwa msimamo wa ligi hiyo.

Kuelekea mchezo huo, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema anatarajia kufanya mabadiliko katika kikosi chake kwa sababu atakosa baadhi ya wachezaji akiwamo Bakari Mwamnyeto ambaye ameumia katika majukumu ya timu ya taifa.

Alisema pia atamkosa kipa namba moja Djigui Diarra, ambaye amechelewa kujiunga kikosini pamoja na Kibwana Shomari anayetumikia adhabu ya kadi za njano.

"Tumejiandaa vizuri dhidi ya Coastal Union kwa sababu ni timu nzuri, lakini pia tunakutana nao mara tatu, kesho tunacheza nao katika ligi, mechi hiyo itanipa mwanga wa michezo ijayo, kwa sababu tunacheza nao katika fainali na Ngao ya Jamii," alisema na kuongeza.

"Kutokana na ushindani wa timu hiyo nimelazimika kukutana na wachezaji kuzungumza nao umuhimu wa mchezo huo na kuwataka wapambane kutafuta matokeo mazuri ili kusherehekea ubingwa kesho (leo)," alisema Nabi.

Naye Kocha Msaidizi wa Coastal Union, Joseph Lazaro, alisema wanaenda kuendelea walipoisha kuhakikisha wanapata matokeo mazuri na kwa kuifunga Yanga katika mchezo huo.

Alisema Yanga haijafungwa katika msimu huu, lakini wamejiandaa kuharibu rekodi ya wapinzani wao hao kwa sababu wamewasoma vizuri na hawakubali kufungwa kwa mara nyingine.

"Tunaingia uwanjani kucheza na Yanga wala si Mayele na Feisal Salum (Fei Toto), wapinzani wetu wasitarajie kukutana na timu dhaifu, tunaenda kupambana kuharibu furaha ya Yanga, tumeona ubora na tumefanyia kazi na kuhakikisha tunarejea Tanga na pointi tatu," alisema Razalo.

Kocha wa makipa wa Azam FC, Iddi Abubakari alisema kikosi chao kipo tayari kwa ajili ya kutafuta pointi tatu muhimu ili kufikia malengo yao ya kumaliza katika nafasi nne za juu na kukata tiketi ya kuwakilisha nchini katika michuano ya kimataifa.

"Hakuna majeruhi kikosi kipo tayari na tunaingia uwanja kwa kuwaheshimu Mbeya Kwanza kwa sababu wako chini ya msimamo, tunatambua utakuwa mchezo wa ushindani na mgumu kwani kila mmoja anahitaji alama tatu muhimu kufikia malengo," alisema Iddi.

Kwa upande wa Mbeya Kwanza, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Aswile Asukile, alisema wamefanya maandalizi mazuri kuhakikisha wanashinda mchezo wao dhidi ya Azam FC.

## MTAJUA HAMJUI....



Straika mpya wa Simba, Moses Phiri, aliyemwagia wino kuitumikia klabu hiyo.

## Simba yaanza mbio ujenzi wa uwanja

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI mashabiki na wanachama wa Simba wakizidi kuwakimbiza watani wao wa jadi, Yanga katika shindano la 'Nani Zaidi' maalum kwa ajili ya kuzichangia klabu zao, uongozi wa klabu hiyo umetembelea kuonyesha jinsi fedha hizo zitakavyotumika kuboresha miundombinu yao eneo la Bunju.

Hadi jana mchana Simba ilikuwa ikiongoza kwa mashabiki wake kuchangia zaidi ya Sh. milioni 105 wakati ikiiacha mbali Yanga ambao walikuwa na Sh. milioni 50.

Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, akiongozana na baadhi ya mashabiki na wanachama wa klabu hiyo pamoja na Msanifu Majenzi (Architecture), Hezron David, jana walitembelea eneo lao la Bunju ulipo Uwanja wa Mo Simba Arena, kukagua na kuonyesha mipaka kabla ya uboreshaji huo kuanza.

Akizungumza na waandishi wa habari katika eneo hilo, Msanifu Majenzi huyo, Hezron alisema tayari wameandaa mchoro na wanaukabidhi kwa uongozi wa Simba na kama ukipitishwa na bodi ya klabu hiyo kazi ianze.

"Baada ya kupata mahitaji kutoka Simba, tumeandaa michoro ipo tayari na leo tumekuja kuhakiki mipaka kuangalia kama inaenda na kwenye mchoro.

"Katika mchoro huu, kuna hosteli ya kisasa kwa ajili ya wachezaji, sehemu ya kulala kwa ajili benchi la ufundi, gym, ofisi, restaurant (mgahawa), Swimming pool (bwawa la kuogelea) na mahitaji yote ambayo yanahitajika kwa mchezaji wa kisasa," alisema Hezron.

Kwa upande wa Barbara, alisema: "Hii kitu ipo ndani ya uwezo wetu, leo tayari tumefikisha milioni 100, hivyo tuendelee kupiga kura kwenye mtandao kwa kuichangia Simba ili tuweze kukamilisha malengo haya."

9 770856 541002 >